My reaction on the local government is that I would like it to be autonomous because this will ease the decision making and implementation of decisions because when the local government decides on certain projects, it takes too long for implementation of that project as they are waiting for the signatory from the Minister for Local Government. Another thing is that the local government officials, the Mayor and other officials in the local government should be appointed by the public and not as it is. This enhances the public participation in the ruling of the local government.

Lastly, I would like the citizens to have a right to disregard their Mayor or their Councillor, whenever he does not fulfil his promises or when he/she becomes corrupt, then the Councillor should be done away with.

Com. Kangu: Frankline Opuko.

Frankline Opuko: My name is Franklin Opuko from St Pauls Amukuru High School, I am in form three. I salute you all. In my views, I would like the new constitution to consider the following views. The current constitution has been allowing members of parliament to carry out their duties but in regard, they have been failing to do so. Therefore, we would like a constitution that will give the citizens a right to do away with non-performing members of parliament, by electing another member of parliament, who will carry out his responsibilities effectively.

Secondly, in the current constitution the members of parliament have been doing their work according to the instructions from their political parties. So we would like a constitution that will enable the members of parliament to do their work according to the instructions from the citizens. One of the objectives of the current constitution is to raise the living standards of its people but it is ironical that the government is not effective in doing this. So we would like a constitution that will improve the living standards of the people. We would also like the President not to influence the citizens to accept his or her proposals, but instead he should allow the citizens to decide for themselves. In this I mean, the President should be neutral. The government should also establish special corruption courts, headed by a reputable judge and to suspend all public officials charged in court overdraft. The current constitution has not reinstated the Chief justice powers to discipline errant members. To ensure that a high standard of discipline is maintained in the judiciary, we would like the Chief justice to be given powers to discipline errant judges and magistrates. That is all.

Com. Kangu: Thank you very much Franklin. Can we have Nicodemus Okwabwai?

Nicodemus Okwabwai: Nafikiri yale yote nilitaka kuongea,

Speaker: Jina lako nani?

Com. Kangu: Imeongewa.

Nicodemus Okwabwai: Mimi ni Nicodemus Okwabwai kutoka hapa. Yale yote nilitaka kuongea yamegusiwa kwa hivyo nina jambo moja tu ambalo ningependa kuongezea. Sisi kama watu wa border, tuko na shida sana, kwa sababu tunashambuliwa. Mara kwa mara tunashambuliwa na wenzi wetu kutoka ng'ambo, wakiwa armed na kwa hivyo tunataka usaidizi. Usaidizi ni upande wa defence. Tunataka, ikiwa itawezekana, sisi tupewe trained homeguards ili waweze kushambuliana na hao majambazi. Hiyo ndio nilikuwa nataka kuongezea.

Com. Kangu: Asante sana.

Speaker: (?)

Com. Kangu: Ngoja tu, nitaita majina. Silvester Siatikho.

Silvester Siatikho: I am Siatikho Silvester from St. Pauls Amukura High school. I am in form three. My first point is about the role of members of parliament. Currently, we have members of parliament who are dormant and they do not perform their roles according to our expectations. This drags behind the social economic development of this country. In refence to this, we would like to have a constitution that lays rules governing the role of ministers or the members of parliament. For instance, if there occurs a decrease in the country's agricultural production due to crop based diseases, then the minister for Agriculture should account for that. We hope that when this is put into consideration with the new constitution,

then the members of parliament will have total commitment to their roles.

Secondly, in the current constitution, it doesn't need one to be a doctor for him or her to be a Minister for health. Therefore, in such cases, problems of mismanagement of various ministries occur. Consequently, we would like to have a constitution that lays rules regarding the appointment of these members of parliament or ministers in particular. To exemplify this, one should have a degree or high education in the areas concerned to the respective ministry for him or her to be appointed a minister.

Currently in Kenya, we have the so-called leaders who we elect. We look at them as our role models. These leaders engage in corrupt deals through which they acquire wealth and presently, such undecorous means of wealth acquisition is not well defined with the law. In the new constitution, we would like such individuals to disclose fully how they acquired their wealth lest they be taken to court and be sentenced accordingly. With that, I would like to thank you very much.

Com. Kangu: Can we have George Otiti?

George Otiti: Kwa majina naitwa George Otiti, mstaafu kutoka kwa wizara ya habari na utangazaji. Mwenye Kiti na ma-Commissioners wetu wa tume, asante sana kwenu kwa kuja hapa leo. Ningependa kuwatumia rambi rambi zetu kuhusu mwenzenu Daktari Ombaka ambaye aliaga dunia. Baada ya hayo, ni maoni yangu kuhusu urekebishaji wa katiba ya Kenya. Naanza kwa kugusa tu kwa kuwa sitasoma zote. Kwanza kabisa nataka kugusa kuhusu maisha ya watu wakongwe, yaani elderly people. Ikiwa baba ama mama hapa Teso ni mkongwe, wamesahauliwa sana kama vile sehemu zingine za Kenya ambapo ,wakongwe wanalindwa sawa sawa kwa kupatiwa utunzaji mzuri, pahali pa kuishi, chakula, mavazi na kadhalika.

Kwa upande wa walemavu, ningetaja machache kuhusu walemavu. Walemavu

wamebaguliwa kwa chochote, wametengwa kutoka kwa watu wazima wakidhaniwa hawajiwezi kufanya kazi ile watu wazima nawaweza kufanya. Kwa hivyo serikali ifikirie kuwasaidia hao walemavu, ili wao pia wajimudu maishani mwao, kwa kifedha na kwa vyombo vya kufanyia kazi ya mikono. Nikigusia kidogo upande wa maskini, Teso ni nchi ambayo serikali imewaacha maskini kabisa, kwani hakuna usaidizi sana kama sehemu zingine nchini. Msaada ukitokea, watu wa kufaidika ni wale kutoka sehemu za bonde la ufa, mkoa wa kati, mashariki na hata pwani, huku, tukijikamua wenyewe. Katika katiba yetu, kuwe na namna ya kulinda watoto haswa mayatima ambao wazazi wao wamekufa.

Kwa upande wa kazi, hapo pia tunabaguliwa. Sijui kama ni kwasababu kabila letu ni ndogo. Kama huna mtu yeyote mkubwa ambaye yuko kwa kazi fulani, huwezi ukapata chochote ama lazima upitie njia ingine ya kutoa TKK, yaani kitu kidogo. Hapo, hakuna cha elimu ambayo wataangalia hapo, kama huna chochote, hakuna cha kupata. Mengine nafikiri mtasoma katika memorandum hii.

Tuwe na viti vilivyotengwa kwa makundi maalum, kama wakina mama, vilema, vipofu na kadhalika. Kuhusu haki ya kimsingi, katiba ilinde haki ya uhai na hukumu ya kifo ibaki vile vile ilivyo. Katiba ilinde haki ya wananchi, kupata elimu ya lazima bila malipo yoyote, kutoka shule ya msingi hadi kidato cha nne. Masilahi ya walemavu yalindwe kwa ukamilifu na katiba. Kuhusu haki ya ardhi na mali, anayepaswa kumiliki ama wa mwisho kabisa ambaye ana haki ya kumiliki shamba ama aridhi ni jamii ya mahali hapo. Serikali haina uwezo wa kutoa ardhi kwa lazima kwa lengo lolote. Cheti cha kumiliki shamba ipeanwe bure bila malipo yoyote. Katiba ihakikishe haki ya kila Mkenya kumiliki ardhi yake. Wanaume na wanawake wasiwe na uwezo sawa wa kumiliki ardhi.

Kuhusu tofauti ya kikabila na kitamaduni, nchi ya Kenya inachangia katika ujengaji wa utamaduni wa taifa na tuwe na lugha moja ya taifa katika katiba na itambue na kuendeleza lugha za kienyeji. Maofisa wa uma ni lazima walazimishwe kutangaza vile walipata mali walionayo.

Com. Kangu: Jaribu kumaliza.

George Otiti: Nikimaliza, kwa upande wa kazi, mtu awe na kazi moja tu kwa kuwa unaweza pata mtu mmoja akiwa na kazi karibu kumi na zote analipwa mshahara. Ni hayo tu na yametayarishwa nami Otiti Christopher George (OCG) kutoka kataya oturu tarafa la Amukura.

Com. Kangu: Gadd Ojala. Wewe ndio mwalimu wa wanafunzi?

Gadd Ojala: Thank you very much. I have the following views to put across.

Com. Kangu: Name please.

Gadd Ojala: I am Gadd Ojala, deputy Head Teacher, St. Pauls Amukura. There is a problem in this district as concern education. You will find that quite a number of kids fail to go to schools because they fail to meet the fees. I suggest that all the civil servants, me inclusive to be taxed some percentage of our pay, that should go to educating of the kids especially in primary and there should be very good accountability of the money that is raised.

On the management of schools, I want to suggest that the PTAs should have an upper hand as compared to the BOG. I say this because the PTA members have their kids in that school and will have the interest of the school at heart, so I think if the PTA is given an upper hand they will actually develop their respective schools.

Lastly, I wanted to talk about farming. In this areas and especially this district, we can boost farming if it is made compulsory. If we use the provincial administration to ensure that each farmer cultivates three quarters of their land and put it into arable use, we can have enough food for this country but looking at the situation at the moment, most people are not very

serious with their farming. Thank you very much.

Com. Ayonga: Bwana Ojala, you said in order to help the poor children who are sent away from school civil servants including you should be taxed. Knowing what Kenya is like and a little while ago we said we are highly taxed than any other person in the world, we are one of the highest and Ojala, you say you are a teacher. You teachers are in the pipeline crying of your salaries, in other words, you are underpaid, that is what you are complaining about. Would you like to suggest how much of tax you would like see done while you are what you are?

Gadd Ojala: I suggest 1% of the basic salary should be taxed from all civil servants and that should go to educate the kids, especially in primary schools so that we can buy basic items like chalk and so on.

Com. Ayonga: Thank you. Next person, do we have someone here by the name Kanoti Isike? I don't know whether you are sticking to one and a half minutes that I gave earlier, Kanoti Isike.

Kanoti Isike: Asanteni sana. Yangu ninapendekeza hivi, kuna makosa mengine ambayo katika katiba ambayo iliendelea, ilionekana ya kwamba kuna makosa ambayo yako juu ya mahakama kwa sababu kuna watu wengine wanaweza kupelekwa jela kabla ya kupitishwa mahakamani. Kwa hivyo ningependa kila kosa, mtu apelekwe na afungwe kupitia mahakamani. Mtu akishikwa, anafaa kwenda remand kwa wiki moja, kwa sababu mtu kama huyu anafaa kuchukuliwa kama hana kosa, mpaka apatikane kuwa na kosa. Watu wa remand huwa wanateswa, wengine wanakufia jela, kama hawana hatia na kwa hivyo tunataka katiba ambayo inatengenezwa iangalie jambo kama hilo.

Com. Ayonga: Unataka watu wawe katika hio jela kwa wiki moja?

Kanoti Isike: Nataka mtu awe rumande kwa wiki moja.

Com. Ayonga: Akiendelea kuteswa?

Kanoti Isike: Hapana.

Com. Ayonga: Eeh?

Kanoti Isike: Asiteswe kwa sababu mtu ambaye atakuwa rumande.

Com. Ayonga: Hatusemi hivyo? Nani aliwauliza maswali nyinyi kutoka huko mjibu? Mimi sijawauliza maswali mnijibu, ni huyu ninaye muuliza. Ungetakaje?

Kanoti Isike: Ningependa, mtu akiwa rumande asichukuliwe kuwa ana kosa kwa sababu huenda hana kosa na anawekwa rumande, kosa lake likichunguzwa. Akipatikana ana kosa, ashtakiwe.

Com. Ayonga: Okay. Endelea.

Kanoti Isike: Hatutaki Wabukusu watutairi, kwa sababu kutairiwa si kimila kwa Wateso kwa hivyo Wabukusu waangalie mila yao, wasitulazimishe kuinga kwa mila yao.

Com. Ayonga: Okay.

Kanoti Isike: Ma-Chief na manaibu wao wajengewe ofisi na serikali, kwa sababu ikiwa Chief wa Nairobi anakaa mahali pazuri, tunataka Chief wa Teso pia, ajengewe ofisi na tukiingia kwa ofisi yake tuheshimu, kwa sababu wengine hawana ofisi mpaka leo. Kama ni Chief wa Kenya, wote wawe sawa.

Com. Ayonga: Okay.

Kanoti Isike: Ni hayo tu.

Com. Ayonga: Asante sana. Wabukusu waacha kuwatairi. Natumaini kama Wabukusu wako hapa wamesikia.

Audience: Ndio

Com. Ayonga: Hiyo haitakikani. Next, huyo alikuwa Kanoti Isike, sasa Ambrose Etyang. Ambrose Etyang, tuambie lile ambalo halijasemwa.

Ambrose Etyang: Bwana Commissioner,

Com. Ayonga: Sema majina yako.

Ambrose Etyang: Ambrose Etyang. Bwana Commissioner, tuna furaha vile mmekuwa hapa siku ya leo. Tutazidi kukupa matatizo yetu. Ministry ya Labour inatakiwa iwe hapa Amagoro, wilayani Teso. Bwana Commissioner, tunataka watupatie court hapa Amukura kwa sababu ilikuwa na mahakama yake na ikahamishwa hadi Busia. Tunaomba Amukura court, tunaomba waturudishie mahakama yetu. Tunaomba tuwe na Amukura Town Council, Angurai Town Council na Chakol Town Council. Malaba iwe Municipality. Bwana Commissioner, wakati huu kuna tofauti ya kijana na msichana. Nikisema hivyo, pengine sijazaa kijana, nimezaa wasichana peke yake. Nikifa, msichana hawezi kurithi shamba la baba yake ama la.

Com. Ayonga: Unatakaje?

Ambrose Etyang: Msichana arithi, mimi nimezaa wasichana.

Com. Ayonga: Ndio. Sema wasichana waridhi mashamba ya baba zao

Ambrose Etyang: Wasichana warithi mashamba ya baba zoa

Com. Ayonga: Endelea.

Ambrose Etyang: Bwana Commissioner, tunataka tupate wabunge watatu, Amukura iwe constituency, Amagoro iwe constituency.

Com. Ayonga: Si hawa wamefika wawili?

Ambrose Etyang: Na Charkol. Bwana commission, tunaomba kila wilaya iwe na mahakama yake. Pia tunaomba Ochofia District hospital, ipanuliwe badala ya kupeleka wagonjwa Bungoma. Ambulance ya Ochofia kuchukua mgonjwa Bungoma, wanalipisha shilingi mia tano, hakuna pesa na hakuna usaidizi katika health centres zote. Malipo ni taabu, tunanunua dawa na hatuna pesa. Hatutaki majimbo, ikiwa majimbo itakuwa sisi Wateso hatutaki, tunaunga central government mkono.

Com. Ayonga: La mwisho?

Ambrose Etyang: La mwisho, hapo awali tulikuwa na paramount Chief Raphael Okisae na sasa wamemsahau na hata jina lake halikumbukwi. Teso district ilikuwa na paramount Chief mmoja na tunataka hio position irudishwe.

Com. Ayonga: Thank you very much. Ujiandikishe kule. Sasa namtaka Pastor Evans Omuse.

Evans Omuse: Majina yangu ni Mchungaji Evans Omuse wa African Inland Church

Amukura. Box 53, Amukura. Ningependekeza wabunge maalum kumi na wawili, wabunge sita wachaguliwe wa kwanza awe kijana, wa pili mama, wa tatu mzee, wa nne Mchungaji, wa tano kutoka kwa makabila madogo na wa mwisho awe mlemavu.

La pili, ningependekeza kuabudu, tuwe na tume maalum, ambayo itaitwa Church Commission na katika hiyo tume, tuwe na waakilishi katika kila wilaya. Pia katika mashirika ya serikali, ya binafsi na pia ya kigeni, tuwe na wachungaji kama washauri wakuu au ma-Councillors. Katika ofisi cha Chief hadi ofisi ya Rais, ambayo inahusika na utawala wa mkoa, ninapendekeza tuwe na wachungaji ambao ndio watakuwa wakikalisha kikao, ili tuweze kurekebisha mambo mengi kwa sababu tunapokuwa na wachungaji, mambo mengi yanaenda sambamba.

Mwisho ningependekeza ya kwamba katika hawa watu kama DC na PS, tuwe na wachungaji ambao watakuwa kati yao, wakati mtukufu Rais anachagua akiwa ndio mwenye mamlaka hiyo, tuwe na mchungaji mmoja.

Com. Ayonga: Ambaye ni nini?

Evans Omuse: Ambaye ni DC, PC na kuendelea hata PS ama minister. Katika wadhifa hizo kubwa, tuwe na mchungaji at least mmoja ambaye ataweza kusaidia zaidi katika mashauri au katika counselling. Kwa hayo nasema mubarikiwe.

Com. Ayonga: Toa hiyo karatasi yako ya (?) Zakayo Soimodoit. Kama nimesema jina lako vibaya, ukuje tu. zakayo.

Speaker: Hayuko.

Com. Ayonga: Okay, sawa sawa. Michael Buramis halafu kuna Jafa Emodi. Jafa naona una maandishi, tunataka tu utumulikie yana nini na pia utuambie yale ambayo hayajasemwa

halafu (?)

Jafa Emodi: Asante sana Mwenye Kiti

Com. Ayonga: Victor Buluma awe karibu.

Jafa Emodi: Wa Tume ya marekebisho ya katiba. Yale ambayo yameandikwa hapa sitaguzia ila tu kuna machache ambayo nitapendekeza, kwa sababu hii karatasi nitawapa ili muende mkasome. Kuna pendekezo ambalo ninapinga katika katiba ya sasa kwamba sheria ya kunyonga mtu itupiliwe mbali. Kwa sababu pengine huyu mtu hana hatia, labda pengine amekosa fedha za kumhonga hakimu, kisha huyu mtu anahukumiwa anyongwe, ilihali inafikia wakati wa kutoa msamaha wa Rais, na inapatikana kwamba huyu mtu amenyongwa. Kwa hivyo nasisitiza sana ya kwamba tume ya marekebisho ya katiba itilie mkazo, ili hii sheria itupiliwe mbali.

La pili, nataka neno democrasia ibainike wazi kwamba ni democrasia. Kwa mfano wale wabunge wetu wanapokuja kuhutubia wananchi ama kufanya campaign, sisi raia ndio tunaumia na tunataka tume ya marekebisho ya katiba, itilie maanani kwamba hawa watu wakienda kuhutubu mahali popote, waende katika team. Kwa sababu wakienda katika team, itazuia chuki, fitina na pia umwagikaji wa damu. Wataenda kama wanasiasa ambao wameelewa democrasia. Kila mara wakileta vifo ni kwa sababu kila mtu anaenda na watu wake na akifika kule anasema muniunge mkono, wale wengine wakija, mpige sasa hivo sisi tunagawanywa katika misingi mbali mbali na tunahimiza tume itilie mkazo kabisa, hao watu watembee katika team, chama cha utawala pia na wapinzani wote, yeyote yule anayetaka kuwaania kiti cha bunge.

Com. Ayonga: Thank you.

Jafa Emodi: La tatu,

Com. Ayonga: Hiyo ni ya mwisho.

Jafa Emodi: La tatu, tunataka Wateso wapeane mfalme wao na huyu mfalme asihusike na serikali, ahusike na Wateso peke yake na achunge kabila la Wateso na sheria zao. Kwa mfano, kuna mila za Wateso ambazo, huyu mfalme akichaguliwa, atahifadhi na kufufua utamaduni wa Wateso. Kwa mfano, Wateso wana maajabu fulani ambayo inaweze kuvutia watalii kutoka nje. Hawa Wateso wanafufua watu waliokufa na kuenda kuwaweka katika mti. Leo huyu mfalme akipatikana hapa, na awe na mahali pake pa kuishi kama makao makuu ya Wateso, ili hawa watalii wakija anawaambia, sisi hapa huu ndio utamaduni wetu na sisi hapa hufufua watu na mahali hapa ndio tunaishi. Unaona watalii wanaweza kuletea Wateso pesa nyingi na hii itafaidi pia serikali.

Com. Ayonga: La mwisho.

Jafa Emodi: La mwisho, nataka kukuhakikishia kwamba Uislamu ni dini ambayo inaabudu Mwenyezi Mungu ila sio dini ambayo inatekeleza ugaidi. Kuna wale wanasema Uislamu ni dini ya ugaidi, wala si wacha Mungu. Kwa hivyo inatakikana itambulike katika katiba kwamba hao Waislamu ni wacha Mungu.

Com. Ayonga: Asante sana. Unasema Wateso wapewe mfalme?

Jafa Emodi: Mfalme

Com. Ayonga: Mfalme anaitwaje kwa Wateso?

Jafa Emodi: Mfalme anaitwa Kabaka.

Com. Ayonga: Kabaka?

Jafa Emodi: Eh.

Com. Ayonga: Hayo ni maoni yake. Asante, ujiandikishe pale. Sasa vijana mnaweza kuona wazee wakiwemo wanakumbuka nasikia. Wazee mnasema anaitwa je?

Audience: Emormor

Com. Ayonga: Emormor?

Audience: Emormor

Com. Ayonga: Sasa mkiseme wazee wasikuwemo, Emormor hiyo itajulikana je?

Audience: Emormor

Com. Ayonga: Emormor?

Audience: Ndio.

Com. Ayonga: Thank you. Next, wapi Victor Buluma? Na baada ya huyo Victor kuna Donald Mac. Nataka utoe lile neno ambalo halijasemwa kama hili la Mfalme wa Wateso limesemwa.

Victor Buluma: Asante sana Bwana Commissioner. Nina machache zaidi hata kama yamesemwa, nitayasema kwa ufupi zaidi kwa sababu yamenichoma tangu.

Com. Ayonga: Unaharibu dakika badala ya kusema hayo uliyonayo. kama yanakuchoma, chomeka upoe.

Victor Buluma: Kwa majina naitwa Victor Buluma, mimi ni mzaliwa wa hapa Teso. Naongea kwa desturi za Wateso. Kwanza, Rais akikosa tunataka pia achukuliwe mahakamani, kulingana na kosa lake.

Com. Ayonga: Hilo tumesikia.

Victor Buluma: Pili, Chief na manaibu wao, wachaguliwe kwa njia ya mlolongo kulingana na mahitaji ya wananchi, ikiwa hawataweza kupewa transfer na serikali. Tatu, liguru ndiye mwanzilishi wa kila jambo lakini anasahaulika. Tunataka apate mshahara kwa serikali.

Com. Ayonga: Hilo limesemwa kutoka aSubuhi.

Victor Buluma: Nne, katika mila za Wateso, tunataka pombe ifanywe halali kwa sababu ni desturi. La tano, wafanyikazi wa serikali wasishikilie kazi zaidi ya mbili, kama ni mingi ni mbili, kwa sababu vijana wengi tumesoma, tumetembea na viatu vimeisha lakini hatuna kazi.

Com. Ayonga: Kwa hivyo unataka je?

Victor Buluma: Tunataka mfanyikazi wa serikali asishikilie kazi zaidi ya mbili ili pia tupate nafasi.

Com. Ayonga: Sawa sawa. La mwisho?

Victor Buluma: La mwisho, wafanyikazi wafisadi, tafadhali serikali isiwape transfer, wafutwe kulingana na makosa yao, ili wengine waichukue wadhifa huo na mwisho kabisa, tunapendekeza, mtu yeyote mzima kuanzia umri wa miaka kumi na nane, akimpa msichana mimba, lazima amchukue na kama sivyo, mimi naona huyo mtu aweze kupeana usaidizi kwa huyo msichana, mpaka atakapo zaa na mtoto afikie umri wa kwenda shule. Kisha amchukue

huyo mtoto, kupunguza garama.

Com. Ayonga: Thank you.

Victor Buluma: Asante sana Commissioner

Com. Ayonga: Donald Mac? Donald Mac?

Speaker: (?)

Com. Ayonga: (?). Pasili Baraza?

Pasili Baraza: Niko.

Com. Ayonga: Mzee tulia hapo. Huyu Donald Mac hayuko kabisa?

Pasili Baraza: Mimi kwa majina naitwa Pasili Baraza Omacharu, retired police officer na Councillor. Maoni yangu ni kwamba sisi Wateso ni watu ambao tunadharauliwa katika Kenya lakini wakati wa kura, sisi pia tuko hapo. Kama uchaguzi uliopita ama wale ambao wako kwa bunge, kama kiti cha President, tulipiga kura kama watu elfu thelathini na sita ya President peke yake. Pia, watoto wetu wanasoma lakini je, mbona sisi tunabaguliwa Kenya? Kama kiti hiki cha Ambassador, hakuna Mteso yeyote ambaye amekaribia hicho kiti na kabila zingine katika Kenya wamenusa.

La pili, kama hiki cha PC, Wateso hawajawahi kupata hicho kiti. Je, sisi ni wakaazi wa Kenya, ambao tumepiga kura au tutasimama wapi?

Com. Ayonga: Hebu nikuambie Mzee, nataka nikusaidie. Sisi usituulize maswali au usijiulize maswali yasio na majibu. Hayo ni mambo ambayo unajua kwamba viti fulani

Mteso bado kanyaga hapo, si ndio?

Pasili Barasa: Ndio

Com. Ayonga: Sasa, tunataka utuambie unatakaje.

Pasili Barasa: Nataka kusema tunataka kiti cha balozi angalau Mteso apate.

Com. Ayonga: Mteso awe balozi.

Pasili Barasa: Awe balozi.

Com. Ayonga: Ndio, hivyo ni vizuri.

Pasili Barasa: Ya pili, Mteso awe PC pia

Com. Ayonga: Awe PC?

Pasili Barasa: Awe PC.

Com. Ayonga: Sawa.

Pasili Barasa: Wateso tuko kwa shida. Kazi ya majeshi, polisi, APs na prison. Kule headquarters inaandikwa siku fulani itakuwa ya kuandika.....

.....*End of tape 5 side A*

Pasili Barasa:.....watu wa army, lakini kuna ubaguzi kama huna ndugu yako na huyu ndugu yako ni pesa na hakuna mtu yeyote aliyechukuliwa kutoka Amukura na Chakori

division. Kwa hivyo naomba, ikiwezekana, serikali ingechukua kutoka kila division, kama watanakiwa watu ishirini, kila division itoe watu kama watano.

Com. Ayonga: Asante sana. La mwisho mzee?

Pasili Barasa: Pia ninasema, kwa Wateso kuna mila ingine ambapo mtu ameowa bibi na pengine amezaa naye watoto wawili, watatu au mmoja na ametoka na kuenda kuolewa mahali pengine na huko amezaa watoto wengine. Baada ya kukaa huko kama miaka thelathini, arobaini ama ishirini, akisikia wewe umekufa na ulikuwa na mali, utaona huyu bibi atakuja na anataka kurithi hii mali na yeye sasa ako na boma mbili. Nataka hiyo maneno iwe katika katiba.

Com. Ayonga: Iwekwe aje?

Pasili Barasa: Iwekwe kuwa yeye ameenda kwa boma lingine kuolewa, asije kufuata kurithi hiyo mali mahali alitoka.

Com. Ayonga: Sasa maliza mzee.

Pasili Barasa: Nikiongeza tena.

Com. Ayonga: Ya kumalizia.

Pasili Barasa: Yangu ya mwisho ni hivi, mtu aki-retire kwa kazi, serikali ikiongeza nyongeza ya mshahara, ingekuwa ikiongeza hata kwa wale ambao wame-retire maana wamesaidia serikali kwa njia mzuri na pengine wanapata pension. Serikali iangalie hiyo maneno.

Com. Ayonga: Hiyo ni point mzuri sana mzee na tumeipata Kenya nzima.

Pasili Barasa: Hiyo ndio yangu ya mwisho

Com. Ayonga: Asante

Pasili Barasa: Asanteni kwa kunisikiza.

Com. Ayonga: Enda kule ujiandikishe. Stanley King'lei? Stanley King'lei ni aje, na afuatwe na Jacob Ekwenye. Tena ningependa kuwakumbusha wale mlio na memorandum, ambao mmekuja nyuma, si lazima wewe ukae hapa na memorandum yako, ikiwa si lazima uje kuongea juu yake. Unaweza ku-Submit your memorandum kule, ujiandikishe, uweke sahihi na utoke urudi nyumbani. We have that provision. Kama una memorandum yako na unataka kui-Submit unaweza kuja straight hata sasa hivi, enda kule ujiandikishe na utoke.

Stanley King'lei: Mimi ni Stanley King'lei na nitazungumzia upande wa Ministry of Education. Unapata walimu wanapata mshahara kutoka kwa education, lakini wafanyi kazi wa shule hiyo hawapati pesa kutoka kwa education. Kwa upande wa health, kuna cost sharing, unalipa pesa na unapatiwa chloroquin ya 30 shillings ile ungenunua madukani. Ukilazwa, unapata hicho kitanda kina watu karibu kumi mna-share kitanda moja na umetoa pesa ya cost sharing.

Com. Ayonga: Kwa hivyo unataka je?

Stanley King'lei: Hapo tunataka maneno ya cost sharing iondolewe.

Com. Ayonga: Okay. Final point?

Stanley King'lei: Nikirudi upande wa commissions, commissions hapa Kenya zimeharibu pesa mingi sana. Hata ukiangalia hilo gari ambalo liko hapo nje ambalo Commissioners' wanatumia, tyre yake peke yake nikiuza, itanilinda miaka zote. Ni hayo tu.

Com. Ayonga: Asante. Utajiandikisha na wakati unapoenda kujiandikisha, ile gari ni ya serikali na tukimaliza kazi hapa kwenu itarudi huko. Pengine ni kwa maana hujui mahali ambapo tunapita, unafikiri ni lami kama hapa. Tumeenda mahali ambapo hata hii gari inashindwa kupanda na gari hiyo imenunuliwa kwa kazi haikununuliwa kwa watu, ni kazi ambayo inafanya. Ikimaliza hiyo kazi, gari inarudi kwa wenyewe. Asante. Jacob Ekwenye, dakika yako moja na nusu ndio utumulikie yale ambayo ulionayo na hawajasemwa hapo mbeleni.

Jacob Ekwenye: Asante. Kwa majina ni Jacob Ekweny. Yale nataka kusema ingawa imesemwa ni kuhusu basic rights. Mtu anaweza kushikwa na polisi na anapelekwa kwa cell na aishi hapo miezi tatu, bila kupelekwa kotini. Unakuta huyu mtu anateswa zaidi hata choo pekee yake ni shida na wanakaa zaidi ya watu kumi na hicho chumba kinafungwa na hakuna dirisha.

Com. Ayonga: Hiyo tunajua. Tuambie kile unachotaka.

Jacob Ekwenye: Sasa mimi nataka choo iwe private, ili mabusu wapate kujisaidia kule nje hapana ndani ya cell.

Com. Ayonga: Cell iwe na choo

Jacob Ekwenye: Private.

Com. Ayonga: Mahali mabusu wanakaa, wakae kama watu?

Jacob Ekwenye: Wakae kama watu wengine.

Com. Ayonga: Sawa sawa

Jacob Ekwenye: Tena, mabusu wanafaa walale kwa matandiko vile wengine wanalala.

Com. Ayonga: Okay,.....

Jacob Ekwenye: Wasilale kwa simiti halafu (?) inachibuka.

Com. Ayonga: Tunaelewa.

Jacob Ekwenye: Yah. Kwa sababu mabusu wanapata shida sana.

Com. Ayonga: Sisi ni Wakenya na tunajua hayo kwa hivyo tuambie tu pendekezo.

Jacob Ekwenye: Pendekezo langu, wanatakikana wapate matandiko, wapate matibabu ya kutosha,

Com. Ayonga: Sawa.

Jacob Ekwenye: Wapate chakula cha kutosha na Commissioners mara kwa mara, wawe wakienda kuangalia shida ya mabusu ndani ya cell

Com. Ayonga: Ndio.

Jacob Ekwenye: Hapana kukaa tu na kuandika, bila kuangalia hawa watu, wanateseka.

Com. Ayonga: Asante.

Jacob Ekwenye: Unaweza dhulumiwa wakati mwingine, unapelekwa kotini na wanakaa miaka tatu rumande. Wakisha kaa miaka tatu, wanapelekwa kotini na wanasema wewe hauna

hatia na unatoka. Sasa, hakuna njia yoyote unaweza kushtaki yule mtu ambaye alikidhulumu ama hakuna njia yoyote ambayo unaweza shtaki serekali.

Com. Ayonga: Kwa hivyo unatakaje?

Jacob Ekwenye: Nataka kuwe na njia ya kushtaki serekali ili ulipwe hizo expenses.

Com. Ayonga: Sawa.

Jacob Ekwenye: Ndio. Tena, kuhusu ukimwi, hili ni janga moja ambalo limeua watu wetu hapa.

Com. Ayonga: Tunajua.

Jacob Ekwenye: Watoto wetu wengi wanakaa nyumbani kwa ajili wanakosa pesa kwa sababu wazazi wote wamekufa. Kwa hivyo naomba serikali ipate njia ya pesa, kama ni usaidizi, utoke huko Nairobi na ifike mpaka kwa Chief, si kwa DO ama DC, ifike mpaka kwa Chief, kwa maana ndio anajua huyu mtu amekufa na ukimwi na watoto wake wako na wapatiwe usaidizi.

Com. Ayonga: Thank you.

Jacob Ekwenye: Yah.

Com. Ayonga: Sasa toa hiyo makaratasi tupatie tafadhali.

Jacob Ekwenye: Ikwishe?

Com. Ayonga: Tunataka kila mtu apate nafasi

Jacob Ekwenye: Okay. Asante's Commissioner.

Com. Ayonga: Nelson Aapa? Ni wewe?

Speaker: Hayuko

Com. Ayonga: Hayuko. Elias Munyane?

Audience: Hayuko karibu

Speaker: Elias Munyane?

Com. Ayonga: Ameonekana?

Audience: Hayuko.

Com. Ayonga: Basi. Tunaendelea. Sebastian Irari. Sebastian Irari?

Audience: Hayuko.

Com. Ayonga: Vitallis Baraza?

Audience: Hayuko.

Com. Ayonga: Bonaventure Omsolo? Yuko?

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Si uje mbele. Nataka utupe memo yako na kama kuna neno unataka kusema la kumulikia, mulika na utupe memo.

Bonaventure Omsolo: I am Mr. Bonaventure Omsolo from Teso County. I had three issues but I realized most of them had been raised so there is not need but jsut to add on, I will talk on local government. I realize in the local government act, as it appears in the constitution, the functions of the Councillors has not been very clear and I suggest that they should be clearly defined in the constitution. As per the functions, which have not been clear, I also suggest that their functions should be clear to foster development in their wards and then there should also be ceremonial policy making. While it has also been a problem between the civic body and the Chief officers, whereby I suggest that, the Chief officers purely remain as implementors of the policies which have been made by the Councillors and secondly should be administrative.

On the same note, as you have always been hearing in the papers, there has been alot of wrangles in the local authorities. As far as that is concerned, I suggest that at least there should be a clear clause in the constitution, on how the indiscipline cases should be dealt with. Also on the same note, though it has not been very clear, I propose the name of the local authorities, especially like the counties, as it is in other areas, it should not be called a district council for the counties. I know I don't have to talk about the stand because alot has also been talked. I know there is need for local authorities to be given autonomy, because as far as the way things are at the moment, the solutions they usually make are not biding because they have to seek for approval from even the minister, but if they are given autonomy, they should be able to make their own resolutions and once they have been made, they should be binding at that particular moment. Also I know we have been having problems in the local authorities and I suggest that we shoul have an independent local authority service commission which will be dealing with the issues pertaining to personnel and admininstrative issues.

On the other hand, I have on basic rights, I know most of the issues have been raised, but I

feel, especially where somebody has been arrested and detained in police custody. If he will be proved not guilty, at least that person should be compensated for damages.

Com. Ayonga: Thank you.

Bonaventure Omsolo: I still have to continue.

Com. Ayonga: You still have (?)

Bonaventure Omsolo: I still have, but I think most of the things that are here, I can just present my memo instead of wasting time.

Com. Ayonga: Thank you so much (?). Victor Omasete. Victor Omasete? Yuko? Do we have.....

Victor Omasete: Niko hapa.

Com. Ayonga: Uko wapi? Dakika moja na nusu. Elikana Oteba? Do we have Elikana Oteba? Omasete endelea.

Victor Omasete: Asante Bwana Commissioner. Kwa majina naitwa Victor Omasete. Niko na maoni yangu na mengine yamesemwa.

Com. Ayonga: Sema yale ambayo hayajasemwa.

Victor Omasete: Ya kwanza, angalau nilikua nataka nifafanue kidogo kwa upande wa Administration, pendekezo langu ni kwamba, elder wa kijiji na Chief achaguliwe na wananchi kwa miaka tano. Hapo tena kwa upande wa administration, upande wa askari, kwa sababu zamani vile askari walikuwa wanatembea na Chief, hatukuwa na shida hii ya uizi ama

matatizo katika kijiji, ndio nilikuwa napendekeza kwa upande wa police, wasiwe wanatembea peke yao katika kijiji, wawe wanatembea na kiongozi wa kijiji. Kwa sababu huu uizi, hata askari naye huwa anapatikana kule na nilikuwa napendekeza ikiwa askari anakuwa suspected katika kijiji, mamlaka iwe kwa wananchi kupata askari peke yao kama wako katika kijiji, bila kiongozi wa kijiji, huyo askari achukuliwe hatua na afutwe kazini.

Com. Ayonga: You have made your point. Askari wakija katika kijiji waje na mzee wa kijiji

Victor Omasete: Ndio

Com. Ayonga: (?) the problem

Victor Omasete: Yah

Com. Ayonga: Enda kwa ingine.

Victor Omasete: Lingine, katika upande wa kazi, mtu mmoja asiwe na kazi nyingi vile imesemwa lakini mtu akistaafu astaafu kabisa na asiwe anataka kazi ingine, kwa sababu kuna vijana ama watoto ambao wamesoma, wapewe hiyo nafasi. Wasiwe wana-retire na anarudi tena kutafuta kazi ingine.

Com. Ayonga: You have made your point.

Victor Omasete: Aki-retire a-retire kabisa. Mtu ambaye amefanya kazi kwa serikali asipate kazi ingine.

Com. Ayonga: Point ya mwisho?

Victor Omasete: La mwisho, mtu mwenye kununua shamba la mwingine, mahali ambapo

anatoka, atoke na barua ya Chief wa area hio na akija kununua mchanga katika area ambayo anakuja na apatikane na makosa kwamba yeye ni mwizi ama ni mchawi katika hicho kijiji, mamlaka ipewe kwa wananchi wa area hiyo, wamfukuze bila kulipa zile pesa alizokuwa amelipa. Hiyo ndio ya mwisho, asante.

Com. Ayonga: Enda ujiandikishe kule. Dismas Ologe? David Aunya? David Aunya?

Audience: Hayuko

Com. Ayonga: Halafu Cornel...

Speaker: Mimi niko.

Com. Ayonga: Wewe ni nani?

Speaker: Josphat (?)

Com. Ayonga: Wewe ni David?

Speaker: I am Joseph (?)

Com. Ayonga: Tuko na Cornel Omuria Karani? Eh?

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Quinto Etyang? Quinto Etyang?

Audience: Hayuko

Com. Ayonga: Hayuko. Benjamin Etianga. Benjamin Etianga? Hayuko?

Audience: Hayuko.

Com. Ayonga: Quintos Achu. Ni wewe? Itika kijana. Akifuatwa na Robert Etyang. Robert Etyang yuko? Kuja hapa mbele. Unaweze kuendelea, Quintos endelea.

Quintos Achu: Thank you Commissioners. I am Quintos Achu. As a Kenyan, I feel that we should have a preamble that states, 'we the people of Kenya declare to live with respect towards each other and recognize our ethnic diversity as an asset and strive to ensure personal dignity to every Kenyan and a right to an economic livelihood and respect for our basic rights to every Kenyan'. To add on that, on the directive principle of the state policy, I feel that we should strive to uphold democratic governance at all times and all issues. Governance to be affected constitutionally.

On constitutional supremacy, it is my mind that amendments to the constitution must involve all Kenyans and not a certain percentage of MPs to vote for amendments. Constitutional select committee, when need arises to be appointed by parliament. On defence and national security, we need transparency in forces recruitment by making open the required figure nationally and at district level so that it should be distributed fairly among all locational levels, to avoid favourism and bias towards other areas. The security unit should be established by the constitution, to avoid (?) from a personal army. There should be a separate defence ministry to check misuse of arms. I feel that a civilian security committee should be established to monitor the arms and the nearby police units together with the DO to check misuse of arms. All arrests should be effected with warrants.

The regular police should be equipped fully with ready up-to-date communication based to police and all localities with accordance with a call of duty. The functions of the APs should strictly be with the provincial administration at locational level according to the Chiefs'

instructions on security matters. Thank you.

Com. Ayonga: Thank you. Enda ujiandikishe kule. Robert Etyang? Robert Etyang, tunataka utuambie yale hayajasemwa.

Robert Etyang: Kwa majina ni Robert Etyang. Nina mapendekezo machache ijapokuwa zingine zimesemwa. La kwanza ni hali ya makesi katika ofisi ya DO, ambazo zinastahili kupelekwa kwa liguru huko kijijini, kwa sababu bwana DO hajui mpaka wangu na wa mwenzangu uko wapi. Kwa hivyo ninapendekeza hizo kesi zirudishwe nyumbani.

La pili, naomba hii mambo ya ID cards iwe ni kitu cha kila siku ili watu wapate vipande kila siku kwa sababu ya masukumano. La tatu ni hii hali ya madhehebu. Hapa Teso, kuna madhehebu mengi na hiki ndicho chanzo cha ukimwi na ninapendekeza ya kwamba wagonjwa wote wa ukimwi wapewe uniform, ili watambulike hao ni wagonjwa.

Com. Ayonga: Nani atalipia hiyo uniform?

Robert Etyang: Serikali. La nne, nataka kuongea juu ya judiciary. Judges huwa retired at 74 years lakini napendekeza waende retire at 50 years.

Com. Ayonga: La mwisho?

Charles Etyang: La mwisho, kuna sheria ambayo iko kwamba mwanamke, kama kwa mfano kama nimeowa mwanamke kutoka Uganda na sheria inasema kwamba akienda kuzalia huko, huyo mtoto ni Ugandan citizen. Napendekeza sheria kama hiyo itupiliwe mbali.

Com. Ayonga: Asante sana.

Charles Etyang: Asante.

Com. Ayonga: Charles Odera.

Charles Odera: Kwa majina ni Charles Ekisa Odera. I have worked with the public service commission as an agriculturalist and I have worked with BAT Kenya. Currently, I am the chairman of Retirees in the district. I have a few points to make. One is the management of our economy. I think the current constitution does not address well how our economy is managed, as we know, our economy is mainly agricultural in nature, even our industries are agro-based. Currently, our farmers are facing unfair competition from outside because of importation of cheap maize, rice and so our own products do not have good market in the country because of that unfair competition.

Com. Ayonga: So (?)

Charles Odera: Sorry. Commissioners, I have the following suggestions to make. One, I would request that in our constitution, the farmer should be protected. Our industries should be protected. Two, the price of inputs currently in the farming industry is very expensive and our farmers cannot afford the inputs. So I suggest, to jumpstart our economy which is agriculturally based, the government should set aside some funds which will go to the farmers through the local authorities as a revolving fund. This is to mainly help the farmers buy inputs. I am sure if we do this, our economy can easily pick up because right now the agricultural sector is almost dead and even the industrial sector.

The second thing I would like to say is this question of local authorities. In the local authorities, I have the following suggestions; I would suggest that the chairman of the local authorities becomes the chairman of DDC. The current chairman of DDC is the District Commissioner and the DC does not come from within the district in most cases and I would suggest that the chairman of the local authority, becomes the chairman of the DDC so that he is aware of what happens in that area. Two, 50% of the members of the DDC should be

locals because they know what they want in that area. Three, this question of language test for MPs and councilors; I think it is not necessary if the minimum qualification is met.....

.....*End of tape 5*

Charles Odera: and it has already been suggested by other colleagues of mine. A councilor or even MP should be above form four and I would urge that it should be a division 4 or D+ with a pass in English. If that criteria is met, then we don't need to test them because already they know the language. I want to go very fast because I have written most of the things. The last thing is about the question of strikes – there are a lot of strikes currently in Kenya. I think the reason is, I have also been affected by the way. The reason is because we don't have a body in Kenya which addresses on the salaries of these people and so I suggest a commission, which I may call Job Evaluation Commission be formed. The work of this commission, is to look at the remuneration of all the government workers and all those in parastatals, so that the salaries are harmonized and this should be a continuous exercise. I am sure if this is done, this question of strikes will not be there. That is what I would like to say. Thank you very much.

Com. Ayonga: Thank you. that is a good point. Now, if you can Submit the memo, it is written?

Charles Odera: Yes

Com. Ayonga: Okay. Submit it. Emmanuel Sokia Omusaka? Silvanus Okia Omukaka? Mark Ejakaiti? Mark Ejakaiti? James Emorut (?) Andrew Oroni? Festo Amoiti? Dakika moja na nusu utuambie lile neno ambalo halijasemwa.

Festo Amoiti: Asante sana Commissioner wetu. Kwa majina naitwa Festo Amoiti kutoka Amukura Division. Maoni yangu ni tatu. La kwanza, Wateso ni maskini zaidi na kitu

ambacho kinafanya sisi tuwe maskini ni rais wetu Moi, kwa sababu tangu aingie kwa kiti, hakuna hata siku moja amekuja kutufanyia harambee.

Com. Ayonga: Hiyo ni point moja.

Festo Amoit: La pili, sisi tukipigana na majirani wetu, inapitia kwa rais wetu Moi kwa sababu amekataa kuamua mambo ya mpaka, kusema mwisho wa Wateso na jirani wenu ni hapa. Sasa anataka vita itoke, ndio atume askari waje wanyanyase Wateso.

Com. Ayonga: Okay.

Festo Amoit: Jambo la tatu, mimi ni mkulima. Sisi wakulima tumepata taabu sana kwa sababu hata tukilima miwa, hatulipwi pesa, tukilima chochote, hata tunapeleka kwa society na hata upande wa maziwa, yote imekwisha. Sasa hii ndio inatuletea sisi wakulima umaskini kwa sababu tumeona watu wanapigania mshahara na sisi wakulima tutapigania nini?

Com. Ayonga: Umetuambia point tatu mzee.

Festo Amoit: La mwisho,

Com. Ayonga: Oh, sasa ni nne

Festo Amoit: La mwisho, sisi ambao tunataka kufanya uchaguzi mwaka huu hatupendelei ya kwamba tuchague mtu kwa sababu ya utajiri wake, labda kwa sababu ya elimu yake, tunataka wananchi wachague mtu ambaye anaweza kuwaongoza, yule ambaye ana kipawa cha uongozi. Mtu anaweza kuwa na elimu lakini hawezi uongozi. Hio ndio ya mwisho.

Com. Ayonga: Asante. Jiandikishe kule mzee. Joseph Omuse. Si tulikuwa na hili jina tena Joseph Omuse.

Joseph Omuse: Joseph Omuse

Com. Ayonga: Ni wewe? Haya, hii nafasi ni yako. Yule anaitwa Josephat Aunya.....

Joseph Omuse: Asante sana mkubwa Commissioner pamoja na wazee ambao....

Com. Ayonga: Sema majina yako

Joseph Omuse: Kutupatia maoni hii.

Com. Ayonga: Majina yako?

Joseph Omuse: Kwa majina naitwa Joseph Omuse Ikaulero. Mimi ni mzaliwa wa hapa Amukura. Pendekezo langu katika hii katiba mpya, ningesema ya kwamba policeman ambaye anashikilia mamlaka ya polisi, angekuwa na namba kwa shati yake. Sio ile namba ya pin, hiyo namba iwe imabandikwa kwa shati yake. Other APs pia wawe na hiyo namba na iwe juu shati.

Com. Ayonga: Hiyo tumeelewa mzee.

Joseph Omuse: Kwa sababu,

Com. Ayonga: Tunaelewa sababu.

Joseph Omuse: Asante. Point yangu ya pili, ningependekeza mashamba, watu ambao wanaweza kurithi mashamba wawe ni wale watoto wenye hiyo boma. Mambo ya mashamba ihusishe watu wa nyumbani kama liguru na wengine, kwa sababu sisi tunanyanyaswa sana kupitia njia ya matajiri ambao wanakuja kunyanyasa na kunyang'anya na kufanya pricing, ili

akunyang'anye hilo shamba kwa sababu wana power ya pesa. Napendekeza mtu arithi shamba lake kwa njia ya kutosha, isio kuwa ya uongo na hio mambo ya mashamba isiende kwa ma-Chief, iende kwa liguru na wazee wa boma.

Com. Ayonga: Sawa. Point ya mwisho?

Joseph Omuse: Ya mwisho, ningependekeza kesi ya mtu ikiwa imeenda kotini ama amepata advocate ama kesi ni yake kivyake, hiyo kesi ifanyiwe uchunguzi kamili ili huyu mtu ahukumiwe. Ni hayo tu, sina mengi.

Com. Ayonga: Thank you very much. Next is Joseph Aunya.

Speaker: Joseph Anunya?

Audience: Ameenda.

Com. Ayonga: Halafu kuna Joseph Kapes.

Speaker: Joseph Kapes (*Teso Dialect*)

Audience: Ameenda.

Com. Ayonga: Andrew Omuruoni?

Speaker: Andrew Omuruoni?

Com. Ayonga: Peter Obuori?

Speaker: Peter Obuori?

Com. Ayonga: Peter, hii nafasi ni yako, toa ile point hatujasikia.

Peter Obuori: Asante sana ma-Commissioners. Langu,.....

Com. Ayonga: Majina kwanza.

Peter Obuori: Kwa majina ni Peter Obouri. Langu la kwanza ni kwa idara ya michezo. Tunataka katiba ya Kenya, kwa sababu michezo imezorota Kenya sana, especially upande wa kandanda, inasaidia serikali kuleta pesa ndogo ndogo. Tunataka katiba ambayo inavyoundwa sasa, coach ambaye atachaguliwa, afike kwa kila district, national coach afike kila district. Pale, tunataka tuwakilishwe kwa kila district katika national team kama Harambee stars, kwa sababu wachezaji wengi wamebakia katika zile tribes ndogo ndogo. Hivi sasa unaona Nairobi peke yake ndio inacheza national team.

La pili, kuna idara zingine za serikali, kuanzia mwanzo hata wakati wa Kenyatta, zilikuwepo. Kuna zingine zimekua mstuni kama Wizara ya (?) ya kutengeneza mabarabara hii, zingine zimekuwa msitu mpaka manyumba imemezwa na nyasi na bado wanakula pesa ya serikali. Tunataka vingine viundwe. Tunataka katiba, kwa sababu watoto hawana pesa ya kusoma, pesa zingine zitasaidia watoto wale maskini.

Com. Ayonga: Sawa. Next.

Petr Obuori: La tatu, tunataka zile tribes' ndogo ndogo pia, wengine watakufa bila kupata minister. Tunataka waakilishwe, wakati Mzee anateuwa minister, President aangalia wengine pia. Minister ana qualification gani ambayo inapitishwa kusema huyu mtu anafaa minister? Inatakikana katiba hiyo iangalie Kenya yote, ili kila upande uwe na minister na ndio kwasababu maneno ikitengenezwa, inapatikana ni sawa sawa, hakuna corruption.

Com. Ayonga: Okay.

Peter Obuori: Asante sana Commissioner.

Com. Ayonga: Thank you

Peter Obuori: Mimi sina mengi.

Com. Ayonga: Enda kule ujiandikishe. Stephen Etyang? Kuna Francis Idewa? Francis Idewa?

Speaker: Yuko hapo nje.

Com. Ayonga: Anafanya nini nje? Sisi tunafanya kazi ndani.

Speaker: Francis Idewa.

Com. Ayonga: Stephen Etyang uko tayari?

Speaker: He is not there

Com. Ayonga: Kuna Crescent Imai.

Crescent Imai: Niko

Speaker: Crescent Imai.

Com. Ayonga: Njoo hapa

Speaker: Etyang amesema alipeana memo

Com. Ayonga: Alipeana?

Speaker: Ndio

Com. Ayonga: Okay.

Crescent Imai: Asante sana Bwana Commissioner. Kwa majina naitwa Crescent Imai na nimezaliwa hapa Teso.

Com. Ayonga: Tuambie maoni ndio.....

Crescent Imai: Maoni yangu Bwana Commissioner, nataka mtusaidie. Mzee kwa boma akifa anawacha watoto, lakini hao watoto wanataka kupata title deed ya hiyo shamba ati waende washtaki kaburi.

Maoni ya pili, katika Kenya nzima, kuna wale watu ambao hawakusoma, lakini wana damu ya siasa na ikisemekana Kenya hii ati kama wewe hukusoma huwezi ukasimama kwa chama chochote ambacho unataka usimame na hukusoma na wananchi wanataka kunichagua, lakini wamenikomesha, sitasimama. Tafadhali Bwana Commissioner, siasi ni akili au siasa ni damu?

Jambo langu la tatu Bwana Commissioner, ningepomba hivi, sisi ambao tunaishi karibu na mpaka, tunaona tofauti ambazo zipo kati yetu na nchi ya jirani na ukienda sehemu za Uganda, unapata watu wamesoma na wako na elimu ya kutosha. Wengine wanasoma kwa njia ya uuzaji wa chang'aa, wamama wanasomesha watoto kupitia kwa chang'aa lakini hapa Kenya wanakata chang'aa ati ni pombe haramu.

Com. Ayonga: Unatake je?

Crescent Imai: Mimi ningetaka mruhusu Kenya iwe kama Uganda.

Com. Ayonga: Hii ni Kenya na hatutaki kufanya Kenya iwe kama Uganda. Tuambie kitu ambacho unataka tufanye.

Crescent Imai: Nataka mlete mtindo kama wa Uganda na iwe hivyo. Kwa sababu ukipata mali pali ambayo iko Uganda, kama hapa Kenya.

Com. Ayonga: Ya mwisho?

Crescent Imai: Jambo langu la mwisho,

Com. Ayonga: Hakuna?

Crescent Imai: Lipo Bwana Commissioner. Unajua vile ulianza kuniuliza, ndio nikaruka.

Com. Ayonga: Endelea.

Crescent Imai: Asante Bwana Commissioner. Sitachosha na mengi lakini ningependelea hivi, kulingana na desturi ambayo iko hapa Kenya, tumeshinda. Ukiwa na kesi na ikichukuliwa kwa DO, bwana DO anakupigisha bei

Com. Ayonga: Eh?

Crescent Imai: Bwana DO anakupigisha bei. Ikiwa kesi imefika kwa DO itakuwa bei ndio inakupiga, badala ya kupeleka kesi kotini. Ukienda police station ukishikwa na wakikuweka pale, unapata bei ndio hiyo. Tumeshindwa koti ni gani na DO ni yupi au police station ndio

gani?

Com. Ayonga: Okay.

Crescent Imai: Bwana Commissioner,

Com. Ayonga: Hiyo unatakaje?

Crescent Imai: Ikiwa mnaweza kutusaidia, mtusaidie katika Kenya hii. Sisi wale ambao tuko nyuma hapa, tunaumia sana.

Com. Ayonga: Sasa sema ya mwisho. Imekwisha?

Crescent Imai: Bwana Commissioner, sitakuchokesha na mengi. Wanatunyanyasa hapa sana. asante sana.

Com. Ayonga: Thank you

Crescent Imai: Oh! Kuna jambo la mwisho. Bwana Commissioner, wengine hapa ni wakulima lakini kulingana na masharti ambayo iko hapa Teso, tunaumia. Hatujui kama President anajua wala hatujui kama mbunge wetu anajua. Ukiangalia hata upande wa ukulima, sisi tunalima tobacco. Unajua kuna wakati ambao tobacco ilikua nzuri, lakini wakati huu ukilima, mvua inakuja kuharibu tobacco na hii ikiharibika na umechukua loan pale, watakuja kushika hata kitanda chako na malazi ndani ya nyumba. Sijui hio ni desturi gani ambayo iko hapa Kenya na tunaomba tafadhali mtusaidie. Asante sana.

Com. Ayonga: Thank you so much. Kuna Josephat Busera. Halafu nataka huyu Vincent Peter awe karibu.

Josephat Busera: Mimi Bwana Commissioner, tuna shida upande wa Teso....

Com. Ayonga: Majina yako?

Josephat Busera: Jina langu ni Josephat Ouma Busera. Shida yetu hapa Teso, kwanza sisi ni wakulima wa miwa na kuna Kenya Sugar Authority ambayo imetoka na tukawa na Sugar Board Authority na wakati walibuni hii Sugar Board Authority mwezi wa nne, walisema kwamba miwa yetu itapimwa ikiwa katika mashamba yetu, ili ikifika kuenda kwa kiwanda, iwe chini ya Kenya Sugar Authority na tunaona hiyo tu ilikuwa ni propaganda na haifanyiki. Kwa hivyo tunaomba kwamba miwa yetu ipimwe katika mashamba yetu, ili hata ikiharibikia njiani iwe chini ya Sugar Board Authority.

La pili ni kulingana na mazingira yetu. Mazingira haya hapa Teso, hatuna ng'ombe. Hii ni kwa sababu ng'ombe ziko, lakini zinakufa bila sisi kujua sababu. Tumeona kwamba haya makaratasi ya polythene, Kenya imekuwa kama dumping place ya polythene papers. Tunaona hawa wafanya biashara wanachukua short cut na hii short cut inaua mifugo yetu. Mama anaenda sokoni, ananunua sabuni na anaenda kufua na kwa sababu hiyo sabuni alikuwa ameeka ndani ya polythene paper, ataenda tu na aanze kufua nguo zake na kuitupa hiyo polythene. Ngombe ikinusa hii karatasi, itakula na ife.

Com. Ayonga: Kwa kifupi unasema polythene papers ziwachwe na tutumie mifuko ya makaratasi?

Josephat Busera: Asante. Hivyo ndivyo tunataka.

Com. Ayonga: Hicho ndicho ulikuwa unataka?

Josephat Busera: Kabisa.

Com. Ayonga: Hebu sema hivyo.

Josephat Busera: Ninasema tuwache mambo ya polythene papers, tutumie kaki.

Com. Ayonga: Okay.

Josephat Busera: Halafu, pia tunaona Kenya tunayotaka ni tupewe elimu ya bure kutoka shule ya nursery mpaka secodary school.

Com. Ayonga: Okay

Josephat Busera: Ya pili,

Com. Ayonga: Ya tatu

Josephat Busera: Okay. Ya tatu, magonjwa. Kuna magonjwa kama kifua kikuu na kweli kama huna pesa ni vigumu kutibu na kwa hivyo tunaomba serikali, ule mwito wa freedom kwamba Kenya tumepata uhuru, tufukuze ugonjwa, tufukuze ujinga na njaa. Kwa hivyo pia tunataka, upande wa agriculture, Kenya hatuna mbegu wakati huu. Hata ukiuliza ma officer wa agriculture hapa Teso, hakuna variety ya mbegu atakuambia ambayo inafanya vizuri na tunajaribu tu kubahatisha. Na tunajaribu kupanda hata na mbolea, haifanyi vizuri na kwa hivyo tungetaka serikali ifanye utafiti wa kutosha na hao ma-officer wa agriculture watuambie ni mbegu gani inafaa katika wilaya ya Teso.

Com. Ayonga: La mwisho?

Josephat Busera: Mwisho nikimalizia, tuko na ndugu zetu polisi na tunawapenda. Lakini ni maajabu kwamba kuna siku nilikutana na polisi usiku wakaniambia mambo ni mawili; usiku ni wa mwizi ama polisi, eti kama wewe si mwizi, wewe ni polisi na kwa sababu si kuwa

mwizi ama polisi, ilinibidi kunyamaza na tulitembea nao sana usiku na ilikuwa mbali na wakasema kuna baridi, kwa hivyo nitoe kitu kidogo ambacho sikutoa. Sasa walitembea nami sana, lakini mahali waniwachia na ilikuwa usiku, ilikuwa mbali na singeweza kuenda nyumbani. Ilinibidi nilale polisi, kwa sababu ya security yangu. Kwa hivyo tunaomba Kenya police wapate training ya kutosha.

Com. Ayonga: Wawache hiyo tabia....

Josephat Busera: Wawache tabia mbaya ya kusema usiku ni wa polisi ama mwizi. Asanteni.

Com. Ayonga: Thank you. nenda kule ujiandikishe. (?) nimesema Vincent Peter?

Speaker: Vincent Peter (emamu)? Hayuko.

Com. Ayonga: Fidel Castro.

Speaker: Fidel Castro.

Com. Ayonga: President wa cuba?

Speaker: Ndio huyu

Com. Ayonga: Ndio huyu? Hata hana jina letu la Wateso? Okay, Fidel tunataka utufanyie kwa ufupi, utuambie yale ambayo wengine hawajasema.

Fidel Castro: My names are Fidel Castro. As pertains to the CKRC, I have the following to pass across. First, pertaining to the Presidential powers, they have to be trimmed. For example, the clause of the President being above the law should be abolished. The

Presidential powers of hiring and firing parastatal heads and Chiefs should be abolished and by so doing, the appointment of all these parastatal heads should be taken over by the Public Service Commission and they should be appointed on merit and not political basis.

Secondly, the judiciary should be streamlined. For example, all dependents and all criminals should be assigned lawyers for justice to all. Security of tenure for those holding public offices should be assured. Presidential appointees for example ministers, parastatal heads, judges and others should be vetted by the parliament to be approved. And lastly, all those responsible for embezzlement of public resources and economic crimes should not be pardoned and should be prosecuted regardless of their political positions in the society.

Com. Ayonga: Na mali walio pora?

Fidel Castro: Yote irudishwe.

Com. Ayonga: Okay

Fidel Castro: Thank you.

Com. Ayonga: Thank you. sasa tuna Jervas Opisi Dindi.

Speaker: Dindi?

Com. Ayonga: Halafu tuna Paul Odeke?

Paul Odeke: Sir.

Com. Ayonga: Paul kuja mbele na Paul anapojitayarisha, Benson Wanjala Imwana?

Speaker: Benson Wanjala Imwana?

Benson Wanjala: Niko

Com. Ayonga: Imwana yuko wapi?

Benson Wanjala: Niko

Com. Ayonga: Kuja hapa.

Paul Odeke: Jina langu ni Paul Odeke na mimi nimezaliwa Amukura. Mimi ni Chairman wa KANU wa hapa, division ya Amukura.

Com. Ayonga: Okay. Endelea.

Paul Odeke: Pendekezo la kwanza, sisi Wateso ni kitu kimoja tu, hakuna kitu cha pili. Kama ndege yangu iko juu ya miti na inataga mayai na kutoa watoto, nafikiri kama hawa watoto wamekuwa tayari, mimi baba wa watoto hawa naweza kuwaonyesha mtu ambaye ninataka. Hakuna mtu anayeweza kupinga ama kuniuliza swali. Swali langu kwa hayo maneno linasema, Mzee wetu Baba wa Taifa ameshachagua mtu, lazima sisi raia, Wateso wa hapa watafuata huyo mtu. Hilo ndilo pendekezo langu la kwanza.

La pili, sisi Wateso, kama msaada unakuja kidogo haufiki kwa raia. Wakubwa wa hapa ndio wanachukua. Kama mkopo unakuja, ile duka imejaa ndio inaingia lakini ndipo yule mtu maskini hawezi kulipa.

Com. Ayonga: Kwa hivyo tufanye nini mzee?

Paul Odeke: Lazima mimi niwape nyinyi report ndio hiyo maneno iweko ndani mtengeneze.

Com Kangu: Mzee wewe unaona shida inatoka wapi? msaada inakuja na inapotelea?

Paul Odeke: Msaada unakuja kwa mikono ya watu wa security.

Com. Kangu: Wakubwa?

Paul Odeke: Wakubwa.

Com. Kangu: Mnh?

Paul Odeke: Na hiyo ikiletwa njaa inawaka kabisa. Kweli hata kama wewe unafikiria, wanaweza kukupa gorogoro moja kwa watu wanne?

Com. Kangu: Unajua shida ambayo tuko nayo mzee, ile sheria ambayo tunapata inasema tuandike katiba ambayo itasaidia kueneza demokrasia kwa sababu uongozi bila demokrasia ndio umeletea watu hii shida unasema, vitu vinakuja, wakubwa ambao hamkuwachagua wanachukua. Na wewe sasa unatuambie turuhusu mtu mmoja kutuchagulia mtu mmoja na sheria inasema tuandike katiba ambayo italeti demokrasia.

Paul Odeke: Ndio. Sasa pendekezo langu hapo linasema, kama nyinyi mnaendele na katiba, ni kitu mzuri kifahamisha wananchi wote ndio sisi tuone kama katiba yenu ni nzuri. Sitaamini, kwa sababu ile katiba inakuja wakati huu, katiba hiyo inataka kuwasaidia wananchi na nini?

Com. Ayonga: Okay. Ya mwisho?

Paul Odeke: Pendekezo la mwisho, katiba hii itengenezwe na sisi tukitaka kufanya katiba mpaka wananchi wakubali hayo maneno.

Com. Ayonga: Ndio maanake tumekuja hapa.

Paul Odeke: Ndio maana mumekuja hapa.

Com. Ayonga: Ndio.

Paul Odeke: Tunawashukuru kwa kufika hapa na kuchukua maoni ya hapa Teso Na ninasema kwa maoni yangu, wale watu wa security wasifanye kama wale watu wanasema tumetoka Uganda kuja kuingilia watu hapa, mahali pao na kusema eti sisi ni watu wa Uganda, kumbe ni watu wa hapa. Huo ndio tunasema lazima kama nyinyi, hii katiba mpya iangalie hayo maneno na ichunguzwe sawasawa. La nne, sisi hapa hatuna mtu ambaye ametusimamia na tunataka mtu atusimamie hatutapoteza morale maanake jirani wetu wanatufinya vibaya sana. sasa vile tulipewa district lakini hatujapatiwa mpaka na hao bado wanakazana. Kwa nini hamchukui Sub-Chief na Chief na kutuambia nyinyi rudini upande huu au nyinyi upande huu? Sasa tunangojea nini, Mzee awache kazi na achague mtu mwingine akuje kuondoa hayo maneno?

Com. Ayonga: Tumesikia.

Paul Odeke: Umesikia?

Com. Ayonga: Ndio.

Paul Odeke: La tano, kama Moi anatuonyesha sisi, yeye mwenyewe aje hapa na mtu wake aje atuonyeshe mtu tutakaye pigia kura.

Com. Ayonga: Sawa sawa

Paul Odeke: Hakuna kusema mtu bure anakuja hapa. Kama Kamotho arudi kwa kiti chake. Zamani huyu Raila, baba yake alikuwa makamu na anaweza kuzungumza ndani ya bunge na sisi tuamini lakini Kamotho arudi kwa kazi yake.

Com. Ayonga: Kazi yake gani?

Paul Odeke: Alikuwa kazi ya kusimamia chama

Com. Ayonga: Mnh. Arudi?

Paul Odeke: Ndio. Sisi hatutaki ubaguzi wa hasira na kuleta watu wengine

Com. Kangu: Mzee akionyesha mwingine badala ya Kamotho?

Paul Odeke: Eh?

Com. Kangu: Mzee akionyesha mwingine badala ya Kamotho?

Com. Ayonga: Tena tukatae?

Paul Odeke: Ndio ninasema Mzee ndio ataendelea na kazi yake mpaka kwa miaka tano kama anafundisha yule mtoto.

Com. Ayonga: Asante.

Paul Odeke: Mzee aendelee?

Com. Ayonga: Aendeleee.

Paul Odeke: Moi mwenyewe, miaka hii?

Com. Ayonga: Tano.

Paul Odeke: Tano kama anafundisha yule mtoto

Com. Ayonga: Ndio

Paul Odeke: Mtoto wa nani? wa kenyatta. Hapana mtu mwingine.

Com. Ayonga: Asante sana. sasa mzee enda ujiandikishe kule. Ulisema wewe ni Chairman wa KANU wa hapa?

Peter Odeke: Ndio Sir.

Com. Ayonga: Thank you. Benson Wanjala?

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Ni wewe? Dakika moja na nusu.

Benson Wanjala: Asante Bwana Commissioner. Kwa majina naitwa Benson Wanjala Imwana. Nitagusia maneno matatu hivi. Kitu cha kwanza, hii katiba mpya ambayo mmleta mumefanya vizuri sana, kwa sababu powers za President, zipunguzwe.

Com. Ayonga: Okay. Lingine.

Benson Wanjala: Sababu ya kupunguzwa ni hii.

Com. Ayonga: Tunajua sababu.

Benson Wanjala: Sababu ni kwamba kuwa above the law na kuna Attorney General ambaye anatakikana awakilishe hicho kiti kama mkuu wa sheria. Kwa hivyo commission iangalie hapo. La pili, inatakikana mtu wa Kenya asiitwe 'mkimbizi' kwa sababu ana ID card ya Kenya.

La tatu, kufuatana na hii katiba mabaya munaunda, ni nzuri kwasababu nafasi ya Sub Chief mpaka kwa PC, raia wanaumia, wakitaka msaada hawapati kutoka kwa hawa watu na wanapata mshahara na afadhali iwe ni kuanzia kwa liguru, Chief mpaka DC wafanye kazi.

Com. Ayonga: La mwisho? Tupe lingine.

Benson Wanjala: Nimefika tatu sasa naomba commission ichukue hiyo maneno nimeongea.

Com. Ayonga: Kuna Charles Oduori. Charles Oduori aje mbele halafu afuatwe na Vincent Adida. Njoo ukae kwa hiki kiti kando ya (?).

Charles Oduor: Asante sana bwana Commissioners na wale wote ambao wanasikiza.

Com. Ayonga: Majina?

Charles Oduor: Kwa majina naitwa Charles Oduor. Neno langu ni moja tu na linahusiana na law courts. Katika law courts, tunatumia lugha ngumu sana ambayo inataka wale wataalamu, yaani professionals wale wanaelewa hiyo lugha. Sasa pale kotini, kuna corruption between the magistrates upto the judges in the high court na upande ule mwingine, wakati mwingine tunakuwa na advocates, ambao wanaelewa hiyo sheria na wameelimika kwa hiyo maneno. Watu wengi wamefungwa na wengine wamekufa kwa ajili ya ignorance.

Com. Ayonga: Kwa hivyo unataka je?

Charles Oduor: Ninawaomba kama wasimamizi wanaotembelea hii tume ya katiba, tuwe na a body ambayo inaweza kuwa enacted ambayo itakuwa independent katika all courts from the district level to the high court. Wakati proceedings zinaendelea in all courts, inakuwa pale independently iki-monitor the progress of proceedings ikiwa inatetea pande zote, kwa defendant na akisikiza vile advocates wanaendelea na hiyo kesi, ikiwa yule magistrate is conducting the case kulingana na ile hali ambayo huwa inatendwa.

Com. Ayonga: Kwa hivyo anakuwa kama kachero?

Charles Oduori: Yeye pale anakuwa kama mtu anasikiliza kujua ukweli uko wapi, so that in case there is any problem, yeye anaelewa. There are times when you realize magistrates come together, magistrates na advocates wanakutana na wanaelewana na mimi niko ignorant about law, I will just be taken and then within sometime nitagundua maneno yamekuwa mabaya na nikienda ku-complain wanasema ignorance has no defence. I had only one point. Thank you Sir.

Com. Ayonga: Okay. Wewe sema majina yako na uendelea

Vincent Adinda: Kwa majina naitwa Vincent Adinda. Nina mambo matatu ambayo nataka ninene ili wewe kama Commissioner na group yake mkaweze kutusaidia. Jambo la kwanza ni kuhusu mambo ya maendeleo. Tunaelewa kuwa uchumi umedhuru kila sehemu lakini jambo la maana ni kuwa tumeona katika Kenya, sehemu nyingi zimeweza kufaidika kutoka kwa hiki kikundi hiki cha NGO. Wamekuwa wakisaidia watu ili kuweza kuinua maisha yao na jambo la kushangaza ni kuwa katika hii familia ya Wateso, wamegandamizwa sana kwa sehemu hiyo. Watu wako chini na si kwa sababu watu pengine hawajasoma lakini inapatikana kuwa wale viongozi ambao wanahusika katika hizi NGO si wa jamii hii, ni watu ambao wanatoka kwa jamii ingine.

Com. Ayonga: Una recommend nini?

Vincent Adinda: Ninaomba kuwa, wale viongozi ambao wako, wasiwe wanabagua, wangeweza pia angalau kuinua Wateso, hasa kwa upande wa maendeleo. Vile tunavyoona kwa Wateso, nyumba zao nyingi ni za nyasi na sio kwa kupenda kwao. Tumeona katika sehemu nyingi, watu wanapewa loan ndogo ndogo, ili kuweza kujenga nyumba ambazo ni za mabati. Wangeweza kupewa loan kama hizi, ili watoke kwa hiyo sehemu ya nyumba za nyasi ili waweze kuishi katika nyumba za mabati, ambapo moto wa gafla usiweze kuwarudhu sana.

Jambo la pili ni kuhusu uongozi. Uongozi wetu, hili jambo ambalo anasema corruption, ni kwa sababu ya watu kutotii. Kwa upande wangu naomba kuwa kama watu wangeweza kutii kulingana na neno la Mungu. Hatungekuwa na hili jambo la umaskini na corruption. Ningeomba kwamba nyinyi kama commission, muwasilishe hili ombi letu kama Wateso. Wale watu wa kuchagua viongozi, wawachague viongozi ambao wanamcha Mungu, wale ambao wanatii neno la Mungu, hao ndio wanaweza kumaliza haya maneno ya umaskini na corruption.

Jambo la mwisho ni kuwa, hata kama limegusiwa nitapitia tu juu na liko upande wa (?). kwa keli, mimi ni kijana mdogo lakini yale mambo ambayo nimepata kulingana na historia ya Wateso, ni kuwa hawajapata kiongozi ambaye angeweza kuwaakilisha na wakaweza kusikika. Jambo ambalo limefanya wasiweze kusikika ni kuwa hawajapewa constituency yao kulingana na umati wa watu. Wamejaribu kuwasilishe hili neno kwa commission, lakini ni kama wale ambao wanahusika wamejaribu kuwanyanyasa. Nashukuru kwa kuja hapa na utaweza kulichukulia hili neno maanani. Wateso wanaomba waweze, hasa watu wa Amukura hapa waweze kupewa constituency yao, sio kuwa hawajasoma. Wateso ni watu ambao wamesoma, lakini jambo ni kuwa wale watu wa kwanza ambao walibahatika kwenda mbungeni, ndio wamekua wakitumia vifua na kunyanyasa wale wadogo ambao wangekua.

La mwisho ni kuwa, katika hiyo sehemu, hawa watu wapewe constituency yao, ili watu wa

Amukura pia waweze kuchagua mtu ambaye wameona anamcha Mungu na anaweza kuwakilisha mambo yao katika uongozi. Ni hayo tu.

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Je, jina lako ni nani?

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Una maneno unayotaka kusema na hayajasemwa?

Peter Ekait: Ndio. Peter Ekait.

Com. Ayonga: Hukuweko wakati tulikuwa. Sema majina (?)

Peter Ekait: Asante sana Bwana Commission. Kwa majina naitwa Peter Ekait.

Com. Ayonga: Okay. Sema hiyo point unataka kusema.

Peter Ekait: Mimi naongea kama liguru. Maoni yangu ya kwanza, tuko na shida sana bwana Commissioner

Speaker: (?)

Peter Ekait: Sasa unapata kwa location ama DO anaweza kuja na sisi hatuna mshahara. Unapata Chief na Assistant Chief wanatuuliza ati tuchange kitu DO anakuja kwa mkutano na sisi hatupati mshahara.

Com. Ayonga: Kwa hivyo unatakaje?

Peter Ekait: Hatutaki hiyo maneno ya sisi kukusanya pesa ama kurudi kwa wananchi, tuwache.

Com. Ayonga: Lakini pia hutaki kupewa mshahara?

Peter Ekait: Tunataka mshahara.

Com. Ayonga: Siuseme hivyo.

Peter Ekait: Cha pili.

Com. Ayonga: Hujasema.

Peter Ekait: Tunataka tupate mshahara pamoja na uniform. Mbona hawa watu wa watchmen.....

Com. Ayonga: Si mbona.....

Peter Ekait: Tunataka mshahara pamoja na uniform.

Com. Ayonga: Haya, point ingine.

Peter Ekait: La pili, kuna mambo ya Madaraka Day, unapata tunakusanya pesa na serikali inaleta pesa wakati wa Madaraka Day, sikukuu hiyo na sisi hatuna namna ya kupata mshahara. Unaona kwa kijiji kingine ni wakongwe tu na wajane na sasa wanasema muende mukusanye pesa huko nyumbani kwa wananchi. Sasa tutapata namna gani hiyo pesa? Hiyo mambo ya kukusanya pesa iwachwe.

Com. Ayonga: Mzee, lakini si umesema hiyo point kwamba habari ya kukusanya pesa iwachwe.

Peter Ekait: Ndio.

Com. Ayonga: Hiyo point imekwisha.

Peter Ekait: Ndio

Com. Ayonga: Sasa unalingine? Mshahara uongezwe na uniform upewe.

Peter Ekait: Ndio

Com. Ayonga: Na habari ya kuchanga pesa iwachwe

Peter Ekait: Iwachwe.

Com. Ayonga: Sasa umebakisha nini?

Peter Ekait: Liguru wana kazi nyingi sana

Com. Ayonga: Hapana. Ndio maana yake utapewa mshahara

Peter Ekait: Ndio. Nafikiri ni hayo tu.

Com. Ayonga: Asante.

Peter Ekait: Asante sana.

Com. Ayonga: Kwa nini kuna mkono juu?

Speaker: Nilikuwa nimechelewa kidogo

Speaker: Hapa mimi nilijiandikisha, huyu (?)

Com. Ayonga: Eh?

Speaker: Nilikuwa nimechelewa

Com. Ayonga: Nyinyi wacheni niendeshe mkutano. Hamjui ninaenda kusema nini.

Audience: Okay.

Com. Ayonga: Kama ulichelewa hiyo ni makosa. Unajua jaji akisimama koti inaendelea?

Audience: Hapa.

Com. Ayonga: Wale ambao mumeinua mikono, hebu inueni tena nione. Mbona hiyo mikono inazidi? Je, mlikuwa mumejiandikisha?

Audience: Ndio

Com. Ayonga: Jina lako litapatikana kule?

Audience: Ndio

Com. Ayonga: Na lisipo patikana?

Speaker: Mimi ni namba mia moja na moja.

Com. Ayonga: Namba mia moja na moja kuja hapa. Wewe namba yako ni gani?

Speaker: Yangu ni 48

Com. Ayonga: 48 songa hapa.

Speaker: Yangu ni 200

Com. Ayonga: Yako ni 200? Na wewe songa hapa. Tena mwingine mwenye namba? Wewe ni namba ngapi?

Speaker: 28

Com. Ayonga: 28? Na ulikuwa wapi?

Speaker: Nilikuwa nimechelewa.

Com. Ayonga: La. Si kwamba ulichelewa, ulienda pahali. Kuja hapa lakini. Ninaweza kuona mtu ambaye hana namba. Mbona unainua mkono juu tena ukarudisha?

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Eh? Si wewe uliongea?

Audience: Aliongea.

Com. Ayonga: Na tena unataka nini?

Speaker: Nilikuwa nimesahau nikiongea.

Com. Ayonga: Hapa, hakuna kusahau. Kama umesahau uje kwa constituency ingine. Ama hilo ulioandika na ulio sahou, upewe karatasi uandike.

Speaker: Haya, leta karatasi.

Com. Ayonga: Eh. Na yule?

Speaker: Sijajiandikisha lakini (?)

Com. Ayonga: Hujajiandikisha?

Speaker: Ndio

Com. Ayonga: La. Hiyo sifanyi. Nyinyi.....

Speaker: (?)

Com. Ayonga: Upewe karatasi uandike kama unataka. Sasa nyinyi ambao mumejichelewesha kwa namna moja ama ingine, dakika ni moja tu na hebu niwambie, nikikuambia unarudia ukubali tu kwa maana maneno yote tumesikia. Nitastajabu kuona mtu akituletea point mpya. Sema majina yako na dakika ni moja.

Timothy Ekesa: Asante sana Commissioner.

.....*End of tape 6 side A*

Timothy Ekesa:.....tena delegate. Kwa hivyo Bwana Commissioner ile maneno kweli mimi nimeona tangu nizaliwe. Nina miaka hamsini sasa. Powers za President zipunguzwe.

Com. Ayonga: Hiyo imesemwa kutoka asubuhi.

Timothy Ekesa:Commissioner, mungeweka sheria ya kusema dini ifanyiwe siku yake peke, siku moja kwa wiki kwa sababu madini yamejaa hapa hata mtu hawezi kulala,wanapiga ngoma na hata kama wezi wanakuvamia, hauwezi kusikia.

Com. Ayonga: Kwa hivyo unataka je?

Timothy Ekesa:Sheria iwe ya kusema mwisho wa dini ni saa kumi na mbili au siku moja kwa wiki kama Jumapili kama sisi Catholic Jumapili.

Com. Ayonga: Na SDA wafanye je na hao wanaabudu siku ya Saturday?

Timothy Ekesa:Ya Saturday ni sawa, catholic pia Sunday yah, halafu hizi zingine za usiku, sheria ingewekwa mwisho wake ni saa kumi na mbili.

Com. Ayonga: Kwa nini hio ya usiku.....

Timothy Ekesa:Ya usiku hii.

Com. Ayonga: Okay, hiyo ni point.

Timothy Ekesa:Ningependa tena, habari ya elimu, mimi nina watoto watatu. Wengine wako primary na wengine secondary. Sheria ingetusaidia sisi hapo, tusomeshe watoto mpaka 8, halafu serikali isomeshe kuanzia form 1 mpaka form 4, kwa sababu hapo ninashindwa kulipa.

Com. Ayonga: Hebu nikuambie, kutoka asubuhi tumeambiwa elimu ya bure, kutoka nursery mpaka darasa la kumi na mbili. Kwa hivyo hiyo tumeshaongea juu yake.

Timothy Ekesa:Kwa hivyo, kweli Bwana Commissioner, kama nikurudia nitarudia. Tuheshimu mila ya watu, culture ya watu tuiheshimu.

Com. Ayonga: Hiyo tumeambiwa.

Timothy Ekesa:Kweli Bwana Commissioner, sisi tumeuza hata ng'ombe hata nini, kwa chakula yako tu na mtu anakuja kukuuliza sasa wewe unafanya nini? Mimi nafanya nini kwa boma yangu saa hii jioni? Wametupa shida hata kuenda ngambo hii na ma-guard wameuwa watu wetu huko, wamechukua maji yaani kuna mto ndogo. Kwa sababu sisi tuko jirani hapa na wale watu wanatengeneza hio kitu mpaka watu wetu wanaenda huko. Tunge ona sheria iwe ikiendelea na hiyo maneno.

Com. Ayonga: Sawa.

Timothy Ekesa:Commissioner

Com. Ayonga: Hiyo ya.....

Timothy Ekesa:Tungepunguza tena powers za wanawake. Wanawake wengi wamepewa kazi kubwa sana. kama unapea mwanamke kazi ya bunge, mwanamke anakaa kwa bunge mpaka usiku, nani atapika chakula? Nani anaangalia watoto? Mungepunguza. Mungewapa kazi mpaka saa kumi na mbili waende nyumbani.

Timothy Ekesa:Okay.

Speaker: Wanasema wazee wasaidie

Timothy Ekesa:Ndio

Speaker: Kupika chakula.

Timothy Ekesa: Hapana, la.

Com. Ayonga: Wewe nilikupa dakika moja na umemaliza mbili tayari

Timothy Ekesa: Asante sana. Bwana commissioner, iko sasa mila nyingine. Kama sisi hapa, pengine sisi hapa kama huyu anapea bibi yangu mimba, hiyo maneno naona ipelekwe kotini. Tungeweka sheria ya kusema rudisha hiyo maneno kwa wazee nyumbani ili atoe *iluku*. Zamani sisi tunaita *iluku*, atoe ng'ombe na kondoo.

Com. Ayonga: Ndio

Timothy Ekesa: Ndio sisi tunatengeneza. Kwa nini tunapeleka kotini?

Com. Ayonga: Sawa. Sasa wewe leta hiyo, tunataka hiyo karatasi. Yule mwingine anaye mfuata?

Timothy Ekesa: Asante sana

Com. Ayonga: Mumeleta maneno mazuri sana.

Anthony Kaptain: Asante sana Commissioners. Kwa majina ni Anthony Kaptain na mimi ni Councilor. Waheshimiwa Commissioners yangu hayatakuwa mengi, manake mengi yamerudiwa na nikiongea pengine nitakuwa narudia mengi, lakini ningependa tu nipeane maoni yangu kuhusu afforestation. Hizi natural resources ambazo ningependelea hasa kwa

Teso, manake milimi yote mkiangalia waheshimiwa Commissioners, kama ungekuja hapa miaka kumi na tano iliyopita, ungekuwa umestaajabu kuona mabadiliko ambayo yako. Kwa hivyo ningependa sheria iwekwe ya kulinda misitu yetu, hata ku-develop misitu ili iwe kielelezo cha watu wa sehemu hii.

Sehemu zingine za chemchemi ya maji, tuna shida kwa sababu wakati huu hapa Teso, land hii imekuwa private one na ningependa regulation, I mean hizi sheria zitolewe na ziwe zinawakilishwa hapa kwa local authorities, ipewe nafasi ya kulinda hizi chemchemi ili isiwe tu mali ya mtu mbapo mtu anaweze kuitumia vile anavyoweza. Ningependa kuwe na hii protection pia. Wakati tulipokuwa tukiongea maneno ya watoto, tuko na shida. Tumesema hao watoto wana wazazi, lakini ni kwa njia gani ambayo tunaweza kuwasaidia watoto? Pendekezo langu lilikuwa ni, local authorities kwa kuwa hao watoto wanatoka hapo, wapewe jukumu la kutenga, kama ni kwa ile mazungumzo yao, watenge kiasi fulani ambacho kinaweza kuwasaidia hao watoto mayatima, ili hii shida ya watoto kurandaranda isiweko. Because ninajua tu ile care ambayo tunaweza kuchukua nyumbani, ndio inaweza kuwasaidia hawa watoto kupata elimu, hawa watoto kupata matibabu, manake kuna watoto wengine ambao tuko nao ambao ni orphans na tukiwawachilia namna hiyo tunapata chokora.

Nikimalizia, ningeguzia upanda wa education. Education hii wakati tulipokuwa tukisoma, kulikuwa na nyakati ambazo tulikuwa na careers. Careers hizi zilikuwa zina-identify mwanafunzi yule angependa kuwa pengine daktari, angependa kuwa nurse ama police. Nafikiri tukianzisha hiyo tena, tunaweza kupata watu ambao watakuwa waaminifu, watakuwa wamejitolea kufanya kazi, kuliko vile tunafanya saa hizi, manake tunachukua nafasi tu kwa sababu hatuna lingine. Nayo hii nafasi pia tukipata lazima iwe ya pesa. Kwa hivyo napendekeza kuwa watoto wanapokuwa na vile wamechagua wenyewe kile ambacho wangependa kufanya, wapewe nafasi ya kuendeleza.

Kwa upande wa administration, ningependekeza tuwe na DC, Chief na tuwe na liguru, maanake hii itapunguza ile duplication ambayo tuko nayo. Kwa country councils wakuwe na

authorities wapewe autonomy ili wapate kujiendelesha kikamilifu. Ni hayo tu ambayo niko nayo Commissioners, singependa kurudiarudia. Asanteni kwa kunisikiza.

Com. Ayonga: Thank you so much. Sasa yule wa mwisho. Sema majina yako.

Andrew Emirone: Jina langu ni Andrew Emirone. Nina points zangu hapa kama nne, tano hivi.

Com. Ayonga: Usirudie ambazo zimesemwa lakini.

Andrew Emirone: Zingine zina.....

Com. Ayonga: Yafaa utuambie zile ambazo hazijasemwa. Kama huyu ametuambia vitu juu ya afforestation na hakuna mtu ambaye alikuwa amesema.

Andrew Emirone: Tafadhali naomba radhi, kwa vile nilikuwa nje sikujua sasa ni gani zimesemwa.

Com. Ayonga: Sasa, ambao tumeita, nikikuambia hiyo imeshasemwa, usiendeleo kuongeza

Andrew Emirone: Okay, asante. sasa point zangu hapa kwa vile nimeandika, ya kwanza nilikuwa nataka kugusa juu ya corruption katika government yetu ya Kenya. mimi naona, Kenya sisi ni tajiri na kama si corruption, hatungekuwa na hii uchumi inaenda chini. Ni kumaanisha hii corruption, kwa maoni yangu ningependelea kama sheria inaweza kuwekwa ya kusema ya kwamba, mtu akipatikana ambaye anaweza kufanya corruption katika serikali na kula pesa ya serikali bila sababu, inatakikana anaposhikwa, mali hiyo yote ambayo alichukua, irudishwe kwa serikali ili watu wengine wafaidike. Sana sana kwa serikali ya Kenya, ni common man ndiye anaumia na sasa hizo pesa zikipotea unakuta mtu amefanya corruption na serikali inamfuta kazi. Inapomfuta kazi anaenda kukalia hiyo mali.

Com. Ayonga: Unataka ifanyiwe nini?

Andrew Emirone: Mimi nataka huyu mtu ashikwe na hiyo mali irudishwe kwa government.

Com. Ayonga: Sawa sawa

Andrew Emirone: La pili, treatment ya serikali katika nchi yetu ya Kenya kwa jumla. Kwa upande wangu sioni ni vizuri. Districts zingine Kenya kuna shida, kwa mfano kama hii district yetu ya Teso tuko na shida. Ukiangalia hii district ya Teso, tuko na mashamba kubwa na machemchemi hizo lakini serikali haiwezi kuja kuangalia hii shamba inaweza kusaidia watu wa Teso, kuleta kama scheme ya mchele, tunaweza kulima na tupate pesa hata ya kusomesha watoto lakini unaona hakuna hatua yoyote ambayo serikali imechukua hapa Teso. Hio ndio ninaomba serikali kama inawezekana, treatment kwa watu wote kama Wanakenya wajaribu kutuangalia sisi Wateso hapa na watuletee industries zozote au project yoyote inayoweza kutuendeleza.

Com. Ayonga: Umesema point serikali ilete industries hapa karibu.

Andrew Emirone: Haya.

Com. Ayonga: Ya mwisho sasa.

Andrew Emirone: Point yangu ya mwisho, lakini sio ya mwisho lakini umesema ya mwisho

Com. Ayonga: Ya mwisho.

Andrew Emirone: Asante sana. Kitu kingine ambacho nimeona, upande wa education naonelea hivi, serikali ingerudisha shule na sisi tulipe school fees, kwa vile ninaona kwa

district zingine kuna shida ya masomo. Unaona mashule zingine zinakuwa equipped vizuri na vitabu na pia mijengo. Kwa maoni yangu, kama serikali inaweza kurudisha masomo ya zamani, watu walipe school fees. Serikali i-equip mashule na vitabu na ma-desk na kila kitu na mtu akilipa pesa na mtoto akienda shule, nafikiri anaweza kusoma vizuri.

Com. Ayonga: Basi. Wewe ume-make point yako kwamba school fees irudishwe wakati watu wengine wanasema tupate free education. Asante. Enda ujiandikishe. Tafadhali.

Andrew Emirone: Asante sana.

Vincent Opuwa: Thank you Mr. Commissioner. I am Vincent Opuwa and I am the leader of the youth in this district. I would like to make some highlights. One, if the....

Com. Ayonga: Did you come late or were you here since morning?

Vincent Opuwa: I was here since morning.

Com. Ayonga: Okay, then you know what has been said and what has not been said.

Vincent Opuwa: Sorry. I have not been very close to the proceedings sir.

Com. Ayonga: Okay, then when I tell you what has already been said, so that we save time.

Vincent Opuwa: I agree with that. Okay. Thanks. One thing I want to mention is that can the constitution help and ban vetting of youth seeking national IDs here in Teso district, the vetting process? Because the youth are (?) stays here and there. Vetting starts from the liguru and his elders, moves to the Assistant Chief and his elders, the Chief and his elders to the DO and his elders. So, if this boy was born from this same community, he has grown up here and he is schooling here or he has dropped out of school, why should he be vetted when he is

seeking for an ID card?

Com. Ayonga: So what do you recommend?

Vincent Opuwa: I recommend that it should be banned by the constitution.

Com. Ayonga: Okay. Next point.

Vincent Opuwa: Something else on the executive, we the youth of this district propose that the Chiefs and their Assistants as it has been proposed, be elected by the common man. We also suggest that they should be transferable to other different places of work for effective and quality services. For you will find this young man is underated in his own community. Old men do not actually accept the young boy like me to be their leader, so there is a tendency or negative attitudes from the elders, towards these young leaders so we are advocating for young turks today.

Com. Ayonga: Okay, next.

Vincent Opuwa: Well, there is an animal in Kenya called corruption. We the youth of this district feel that there are some areas, if the constitution can guide and protect, will be reducing corruption in Kenya. one is the Ministry of Health. If the constitution can ban all private hospitals, clinics and chemists, we will have quality services in the government institutions. For this reasons we said is that, you will find that if drugs are brought into a hospital, the very doctors who work there have private clinics somewhere and private chemists. The drugs disappear in a very few days to those personal institutions and if you go to hospital you are told, there are no drugs here and you are referred to a private clinic somewhere, to a private chemist somewhere and the drugs are from this government institutions.

Com. Ayonga: So what is your recommendation?

Vincent Opuwa: I recommend that all private medical institutions be banned by the constitutions.

Com. Ayonga: All private?

Vincent Opuwa: Medial institutions.

Com. Ayonga: Be banned?

Vincent Opuwa: Yes.

Com. Ayonga: That is your recommendation. Next and the last.

Vincent Opuwa: Second last, sorry. Last but not least, this land and property rights. As I mentioned earlier on, I also recommend here that private land surveyors also be banned by the constitution because the reasons are the same as I mentioned about the ministry of health. In winding up, this is about the judiciary. The same applies. If you are targeting to do away with this animal I am calling corruption, we should not have advocates in Kenya because the government already has judges and magistrates then why should we then extend hand having private lawyers? These are the people who are causing corruption. Allow me on one minute to give an example. I witnessed a case, a person killing another, he was arrested and taken to the police station and he is remanded. But because this man, the murderer here, has money and advocates, he was able to hire an advocate. The case went on and the man was still in remand and it was reduced to manslaughter. After some time the man was released, claiming that there was no evidence. Supposing this advocate was not there and we held the government magistrates or judge, whom could this man have hired to reduce the case from murder to having no evidence? Therefore, I recommend the idea of advocates be abolished in Kenya.

Com. Ayonga: In other words you say we abolish the Kenya School of Law.

Vincent Opuwa: No really the school of law.

Com. Ayonga: Why should we take our boys and girls to.....

Vincent Opuwa: Maybe what.....

Com. Ayonga: To the university and they study law then they go to the Kenya School of Law.

Vincent Opuwa: What I would like to say is this, if our Kenyan young boys and girls go to the university or to the school of law and thereafter, they should be accommodated by the government.

Com. Ayonga: Thank you. Those are your recommendations. One question .

Com. Kangu: Why will you want people to elect Chiefs and Assistant Chiefs? I would think because people want to be ruled, by people they have elected themselves. If that is the reason, why will you elect your Chief in Amukura, then tomorrow he is transferred to Chakol, and you are brought someone you didn't elect.

Vincent Opuwa: Personally as I said the transfer of Chiefs and their Assistants, I still recommend that. The community elects these leaders, but not all of you in that community will accept and like this man and his services. As with the little experience I have gathered, we Africans and let me say maybe we Tesos, they value most services from a foreigner but not an indigenous person from that community. So if somebody is posted from Chakol to work here in Amukura, they will respect and honour him and his services than me who was born and grew up in this community, I school here, people know my reputation whether it

may be bad sometime, but they will not accept me fully.

Com. Ayonga: The bible says a prophet will not be respected in his own country.

Vincent Opuwa: Even Jesus was denied in his own community.

Com. Ayonga: Yes but he still became the Saviour of this world.

Speaker: (?)

Com. Ayonga: I think I am coming to the end of this session. Kuna aliye na swali? Thank you. now, on behalf of my colleague here Commissioner Kangu na staff yetu ya secretariat, I want to take this opportunity to thank you the people of this place. It has been a very interesting sitting that we have had here in your place. We have had very many and different views from all of you. You noticed in the morning and during daytime, noon and afternoon, we were full to capacity and then we had an overflow through the windows and out there and you have all listened very carefully and I think we have listened to you too, very carefully. If we didnt listen, then that ka-machine has done its best for what it was created for. Now, first I want to thank those of you who prepared this place, the District Coordinator, your team of 3Cs, the Provincial Administration which even if they say, Bwana Senior Chief kwamba mtolewe kazi mchaguliwe na watu, mumefanya kazi nzuri kwa kushirikiana nasi CKRC kwa kuweza kufanya this possible. Tumetosheka na tunawashukuru nyote na nyinyi pia kwa kuwacha kazi zenu na kuja hapa. Mimi kama mtu ambaye amekuwa hapa kwa mara ya kwanza, nimejifunza machache lakini mengi pia, kwamba hapa Teso mambo yako hivi na vile. Pia nikaja nikapata tumeoa msichana wenu, kwa hivyo nikija hapa muwe munaniheshimu kama shemeji. Tutaona huyo msichana utamaduni ambazo amebeba kuenda huko, nikimpata nitamuambia kule wanatunza utamaduni wa Kiteso na wewe tunza zetu hapa, lakini sisi tunasema mtoto ni mtoto, awe ni msichana ama ni wa kiume, kila mtu apatiwe haki yake. Mzazi ni mzazi wa wote na watoto ni Mungu ametupa, ni baraka kutoka kwa Mungu na tusije

tukawabagua hapa katika hali yetu ya, sijui tunaiita nini. Hii habari ya kuwa ni mbanifu kwa kutoa kitu ampe mwingine, anajifikiria sana, self considerate. Unajifikiria peke yako, na hawa watoto matunda yako unaanza kuyaona ni mengine, hebu tuwaangalie wote.

Zaidi ya yote, constitution yetu iwe na kazi ya kutuunganisha Wakenya kuliko kutugawanya. Kama constitution haiwezi kutuunga tuitwe Wakenya wala sio Wateso au Wakisii au Waluhya au Wajaluo, basi hiyo haitakuwa constitution nzuri. Constitution ni ile ya kunifanya nikikuona, naona ndugu yangu, naona dada yangu, naona shemeji yangu, tutakula pamoja na tuishi pamoja anywhere in Kenya without being discriminated. Constitution yetu iwe ndio dawa ya kuua ukabila na kuua unyumba, kuua clanism ndipo tutakuwa na constitution nzuri. Lakini hayo yote tutayafanya ikiwa Mwenyezi Mungu atatupa ule uwezo na tukimuangalia yeye tukijua sisi wote after all, when all is done sisi ni wana na binti za Mungu. Hatuwezi kuenda ile mbingu ambayo tunatazamia kama hapa duniani tunaangaliana na macho, nikikuona naangalia pande ile au nikipita najifanya sikukuona nakazana kuenda pande hii, hatuwezi kuuona ule mlango wa mbinguni hata kidogo. Lazima tuwe na mbingu mpya hapa duniani. Lazima tufurahiane kwa kukutana na kusema oh! Nime miss kuenda huko Amakura. Kule Amakura kuna watu wangu huko, marafiki zangu, ndio tukikutana mahali fulani, tunakumbatiana kwa salamu na kufurahiana. Je, una neno la kusema wewe Bwana District Coordinator? Una neno kidogo? Ndio maana useme hilo neno na ili Senior Chief atufungie mkutano, kwa maana yeye ndiye ametulinda hapa siku nzima, akatulisha, ametulinda hapa ki-security na chairman naye aseme mawili ndipo tuombe tutoke.

Charles Ekesa: Asante sana Commissioner Pastor Ayonga. Ningechukua nafasi hii nitoe shukurani zangu nyingi kwenu Commissioners na team yenu yote ambayo mumekuja nayo. Nafikiri kwangu kazi nzuri imefanyika na ningeshukuru sana wale wote tumesaidiana nao kufanikisha hivi vikao, ambavyo vimekuwa katika wilaya ya Teso. Nafikiri tumeridhika kama Wateso kwamba, commission yenye imeteuliwa kuangalia mambo ya katiba imefikiria vizuri na kazi ambayo nyinyi Commissioners mmefanya, tumeona kwamba mmekuwa wanyenyekevu kabisa, ingawa wakati mwingine tumekuwa na vikwazo hapa na pale,

nimeona ya kwamba mmefanya kazi nzuri sana. Shukrani kwa wale wote ambao wamesaidia hasa provincial administration wamewezesha kazi yetu kama district coordinators, kuwa rahisi sana.

District Social development office pia imesaidia sana. Ukiona hall kama hii iko katika mikono ya District Social Development Office na wamesaidiana sana na sisi kufanikisha kazi hii. Asanteni sana kwa jumla kwa kazi nzuri mmefanya. Sasa chairman wa CCC atasema jambo na Chief wetu atatufungia mkutano wa leo. Ningeomba mmoja wetu Chief akimaliza, atuweke mbele za Mwenyezi Mungu, kwa sababu nafikiri kwamba sio kwa upendo wetu ati tumeweza kukaa hapa na kumaliza vizuri, ni kwa upendo wa Mungu. Ningeomba mmoja wetu aweze kutuweka mbele ya Mungu. Asante.

Samson Olubayi: Mimi kama chairman wa CCC, langu litakuwa fupi. Kwa upande wa commssioners, sisi kama wakaazi wa hapa tumeridhika na ile kazi mumejanya, kwa sababu tangu juzi, Malaba, Chakol mpaka leo, wakati mwingine mimi, kama mzee wa hapa ambaye nina hasira, wakati mwingine hawa watu wangu wanapotoa maneno hivi ningelisema hapana, hapana fanya hivyo, lakini ni maajabu you have been accomodative kwa chochote ambacho wakaazi wamejaribu kusema, umejua kitu cha kufanya. Tunashukuru zaidi kwa jinsi umetupa hiyo nafasi.

La mwisho ni kwamba, kwa upande wetu wakaaji wa hapa, letu kama committe yenu, tunashukuru. Singekuwa na furaha kama pengine ikiwa saa nane, hawa Commissioners wanakuwa watu ambao wanauliza sasa wapi watu ambao tungeongea nao au wangetupa mawaidha. Wingi wenu na hata Commissioners nawaambia, kama ingekuwa kupeana dakika tano, najua tungeondoka hapa mid night, lakini kwa sababu ya kupunguza kama ilivyoanzishwa, tulipoanza kulikua na formula kwamba ikifika afternoon tutapunguza. Kama haingekuwa hivyo, tungekuwa na nafasi kidogo zaidi. Nawashukuru wananchi kwa kuja kwenu na viongozi mbalimbali. Mwisho, kwa upande wa provincial adminstration, Bwana Senior Chief utapeana shukrani zetu kama committee kwa ofisi ya DO kwamba tumeshukuru

zaidi kwa coverage ambayo mmetupa kwa njia mbali mbali. Kwa hayo, nashukuru na kukuuliza useme moja au mbili. Asante.

John Ikokonyi: Commissioners wetu, Coordinator, Chairman na viongozi mbali mbali, mimi pia nachukua hii nafasi, kutoa shukrani zangu kwa niaba ya division, kwa Commissioners kwa kukaa na kuchukua maoni ya watu tangu asubuhi mpaka wakati huu. Asanteni sana, mmefanya kazi nzuri. Na kwa wananchi ambao wamekuja hapa kutoa maoni yao mbalimbali, pia nataka kutoa shukrani kwa sababu ya kuja nakutoa maoni. Najua tumezungumza na ni jukumu la ma-Commissioners sasa kuenda kuweka maoni yetu kwa sheria. Kwa hivyo, mimi kwa niaba ya DO, ningependa kusema asanteni sana ma-Commissioners, officials kutoka commission, chairman, coordinator na wote ambao mumekuja hapa. Asanteni sana. May God bless you, thank you very much.

Charles Ekesa: Mtu moja ambaye anaweza kutuomba? (*aji ni ebeikini agamakini oni*)

Samson Olubayi: Hebu tupate kuomba, naomba nyinyi nyote msimame. Wale wakatoliki (na wengine?)

Kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, amina. Ee Mungu Baba Mwenyezi, tazama wakati huu ambapo tumefikia kikomo. Ee Mungu Baba Mwenyezi, tungependa kukurudishia shukrani, kwa maana umekuwa nasi mwanzo wa mkutano huu wetu. Ee Mungu Baba Mwenyezi tunasema ni asante na shukrani sana. Ee Mungu Baba Mwenyezi yote ambayo tumeongea hapa, Ee Mungu Baba Mwenyezi uweze kutuma roho wako Mtakatifu ili atangulie mbele ili yote yapate kutekelezwa. Ee Mungu Baba Mwenyezi, wale wote ambao wametoka mbali hasa ma-Commissioner na wale wote wa Constitution Review ninawakabidhi mikononi mwako, ili uweze kutuma roho wako mtakatifu aweze kuwa nao ili aweze kuwalinda wasafiri salama, wafike na wazidi na kazi yao pamoja na roho mtakatifu. Tunaomba hayo yote kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, amina.

